



**MUONGOZO WA KUWEKA NA KUSIMAMIA
MALI ZA WAKFU
ZANZIBAR**

**Umeandaliwa na
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amane
Zanzibar**

Muharram 1435/Novemba 2013

DIBAJI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

Muislamu anapotangulia mbele ya haki; huku nyuma pengine huacha mali ambayo yeye mwenyewe alikusudia kutoa kuwa katika sadaka inayoendelea, ili imnufaishe hapa duniani na huko akhera tunakokwenda. Mali kama hii ambayo muekaji huiweka katika dhima ya Subhanahu Wataala ili isije kumilikiwa na mtu mwengine yeyote huitwa kwa misingi ya Kiislamu **“Mali ya Wakfu”**.

Mali hizi huwa aina mbili, ile inayohamishika na ile isiyohamishika. Katika kutekeleza maagizo ya mja ambae mali yake ameiweka wakfu kuna mambo mengi ya utaratibu wa kufanya na kufuatwa ambao utahalalisha mali hiyo kukidhi haja ya kuitwa mali ya wakfu. Lengo kuwa ni kuleta maendeleo ya jamii ya Kiislamu na kuwasaidia wahitaji katika kuzikurubisha hali zao. Sunna hii kubwa inapotekelawa kwa nia safi basi inamfanya muhusika awe karibu sana na Muumba wetu Mtukufu, Subhanahu Wataala.

Kitabu hichi kidogo kimesheheni elimu hiyo ya Wakfu, kimeelezea malengo yake, historia yake na vipi inavyotekelawa hapa Zanzibar na namna ya kuusimamia wakfu huo. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ikiongozwa na Sheikh Abdulla Talib Abdulla, katika kitabu hii wanaelezea kwa undani hekma za kuletwa kwa Sheria ya Wakfu ambapo mja hunufaika na mali yake hata baada ya yeye kurejea kwa Mwenyezi Mungu wetu.

Wakati huo wale wote anaowapenda kama vile jamaa, masikini na kadhalika huwa bado wananaufaika na marehemu mja huyo. Hekma hii ya Mwenyezi Mungu inazidi kutufundisha kuwa Mwenyezi Mungu anatupenda sana na ametuonesha kila aina ya njia ya kumcha ili tupate radhi zake na tuweze kupumzika pema huko akhera. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana wamefichuwa ukweli huo katika muongozo huu wa kuweka na kusimamia mali za wakfu. Ni muhimu kwa kila muislamu kuusoma na kuuelewa.

Jee wakfu unaweza kubadilishwa? Nini hasa kinachoweza kuwekwa wakfu, na sharti zake ni zippi? Vipi wasia nao unaweza kuelezea habari za wakfu? Ni baadhi ya mambo ambayo yanazidisha elimu hii muhimu katika muongozo huu. Muongozo huu hauishii hapo, lakini pia kuna wajibu wa taasisi pamoja na watu wanaosimamia wakfu unaohusika.

Muongozo unaelezea wazi namna ya kutoa huduma hizo, kuziendeleza mali zake na kukuza mapato yake na kwa maana hiyo kujenga imani kwa wananchi katika usimamizi wa vyombo vinavyohusika.

Wengi hatuelewi kama fedha taslim nazo zinaweza kuwa wakfu. Muongozo huu pia unadondoa hali halisi ya utaratibu unaohitajika kwa fedha hizo. Hii ni elimu ambayo kila mtu anapaswa aijue.

Wakfu unatakiwa utunzwe, usimamiwe ipasavyo na usitumiwe vibaya. Ni kosa kubwa kuutumia vibaya na kinyume cha matakwa ya mueka wakfu. Ni ombi langu kwa wasomaji wa muongozo huu kuwashajihisha na wengine wausome ili na wao waelewe maudhui hayo. Kufanya hivyo ni kukumbushana na hivi ndivyo tulivoamrishwa: ***"Na saidianeni katika wema na kumcha Mwenyezi Mungu"*** Al-Maida aya ya 2.

Kwa kuzingatia kuwa Zanzibar ni mionganoni mwa jamii zenye Waislamu wengi ambapo shughuli za Kiislamu ikiwemo Wakfu huchukua nafasi kubwa katika maisha ya kila siku. Hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa msukumo wa kuimarissha na kujumuisha taratibu za Kiislamu katika mipango na mikakati ya kitaifa ikiwemo Dira ya 2020 na MKUZA kwa lengo la kukuza Uchumi, kupunguza Umasikini na kuwawezesha waumini wajikurubishe zaidi kwa Mola wao.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie sote tuwe katika njia iliyonyooka. Aidha Sote tuweze kuusoma Muongozo huu muhimu pamoja na miongozo mengine yenye lengo la kunyanyua dini yetu ya Kiislamu. Inshaalla Mwenyezi Mungu awalipe wale wote waliojitlea kuifanya kazi hii na Inshaalla kazi hii iwe ya kheri na iweze kunufaisha waislamu na wananchi wenzetu wote. AMIN.

Abubakar Khamis Bakary
Waziri wa Katiba na Sheria
Zanzibar

SHUKURANI

Shukurani zote anastahiki Mwenyezi Mungu ambae kwa neema zake hukamilika mambo mema. Kuikamilisha kazi hii kumetokana na juhudhi na mchango mkubwa uliotolewa na watu na taasisi mbali mbali. Kwa kuitikia kauli ya Mtume SAW “Hamshukuru *Allah asiyewashukuru watu*”. Tunatoa shukurani zetu za dhati kwa wote. Nafasi haitoshi kuwataja wote kwa majina lakini Mwenyezi Mungu anawajua na atawalipa.

Shukurani maalumu ziwaendee Bodi na wafanyakazi wote wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Wizara ya Katiba na Sheria, Taasisi ya “*Waqf South Africa*”, Sheikh Nassor Ameir Tajo, Hajjat Mtumwa Khatib Ameir, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar ndugu Juma Amour, Mhandisi Khalfan Khalfan, Sheikh Shamim Khamis Machano, Bi Mwanaidi Shah, Maalim Mohammed Ali Ugoda kwa ushauri na michango yao iliyoifanya kazi hii ionekane katika hali njema kabisa na kutoa faida kwa mujibu wa mahitaji ya wakati tulionao.

Tutakuwa wezi wa fadhila iwapo hatutamshukuru Mshauri Mwelekezi wa kazi hii, ambae pia ni Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Sheikh Abdulla Talib Abdulla, pamoja na familia yake kwa kuifanya kazi hii kwa kujitolea wakitarajia radhi za Allah. Tunatambua wamejinyima muda wao mwangi wa mapumziko na kutumia nyenzo na rasilimali zao nyingi katika kuhakikisha kuwa kazi hii inakamilika.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mola wa Arshi iliyo kuu aijaalie kazi hii iwe ni khalis kwa ajili yake, awalipe wote waliosaidia na watakaosaidia kwa namna yoyote malipo makubwa duniani na akhera na aijaalie iweze kunufaisha umma wa Kiislamu. Amin

Dr. Issa Haji Ziddy,
Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi,
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.
Zanzibar.

YALIYOMO

DIBAJI

SHUKURANI

YALIYOMO

SURA YA KWANZA : UTANGULIZI NA USULI

- 1.1 Maana ya Wakfu
- 1.2 Malengo ya Wakfu
- 1.3 Historia ya Wakfu
- 1.4 Historia ya Wakfu Zanzibar
 - 1.4.1 Usimamizi wa Wakfu Wakati wa Sultani (1832 – 1890)
 - 1.4.2 Usimamizi wa Wakfu Wakati wa Waingereza (1890-1963)
 - 1.4.3 Usimamizi wa Wakfu Kuanzia Mapinduzi ya 1964 hadi 2007
 - 1.4.4 Usimamizi wa Wakfu Kuanzia 2007 hadi Sasa.
- 1.5 Makusudio ya Muongozo

SURA YA PILI: MAELEZO YA WAKFU NA MISINGI YAKE

- 2.1 Asili ya Sheria za Wakfu
- 2.2 Hekma za Kuletwa Sharia ya Wakfu
- 2.3 Aina za Wakfu
- 2.4 Nguzo za Wakfu
- 2.5 Namna za Kuweka Wakfu
- 2.6. Wahusika wa Wakfu
 - 2.6.1 Muweka Wakfu (*Waqif*)
 - 2.6.1.1 Sharti za Muweka Wakfu
 - 2.6.1.2 Haki za Muweka Wakfu
- 2.6.2 Msimamizi wa Wakfu (*Mutawali*)
 - 2.6.2.1 Usimamizi wa Mali za Wakfu Kitaifa
 - 2.6.2.2 Uendelezaji wa Mali za Wakfu
 - 2.6.2.3 Wanufaika wa Wakfu (*Beneficiaries*)
 - 2.6.3.1 Aina za Wanufaika
 - 2.6.3.2 Namna ya Kunufaika na Wakfu

- 2.7 Kilichowekwa Wakfu (Mawquuf)
- 2.7.1 Sharti za Kinachowekwa Wakfu
- 2.7.2 Umiliki wa Mali iliyowekwa Wakfu
- 2.7.3 Kubadilisha Mali ya Wakfu (*Tabdil*)
- 2.8 Masharti ya Ujumla katika Wakfu
- 2.9 Sura za Wakfu
 - 2.9.1 Wakfu Unaotokana na Wasia
 - 2.9.2 Wakfu wa Mali Isiyohamishika (*Waqf of Remainder Estate*)
 - 2.9.3 Wakfu wa Fedha Taslim (*Cash –Waqf*)
 - 2.9.4 Wakfu wa Mapato ya Mali (*Income Property*).
 - 2.9.5 Wakfu wa Utumizi wa Majengo (*Real Estate Waqf*)
 - 2.9.6 Wakfu wa Familia
- 2.10 Uhustiano na Tofauti Bainya ya Wakfu na Wasia (*Will*)
- 2.11 Uhustiano na Tofauti Bainya ya Wakfu na Amana (*Trust*)

SURA YA TATU : MAHITAJI YA MABADILIKO KATIKA WAKFU

- 3.1 Utangulizi
- 3.2 Wajibu wa Taasisi Zinazosimamia Wakfu
- 3.3 Sababu Zinazoathiri Uendelezaji wa Wakfu
- 3.4 Vipaumbele Katika Uendelezaji wa Wakfu
- 3.4.1 Mambo ya Kutekelezwa kwa Haraka
- 3.4.2 Mipango ya Baadae ya Utekelezaji
- 3.5 Taasisi Zinazotoa Misaada ya Kitaalamu na Mitaji ya Wakfu
- 3.6 Mambo Muhimu ya Kuzingatia Katika Kuomba Miradi
- 3.7 Miongozo Inayohusiana na Kodi
- 3.8 Nyenzo za Mafanikio katika Shughuli za Wakfu
 - 3.8.1 Dira na Uongozi:
 - 3.8.2 Uhamasishaji wa Wadau na ushirikishwaji
 - 3.8.3 Umilikishwaji wa Jamii
 - 3.8.4 Sera na Sheria zinazotoa nguvu kwa Shughuli za Wakfu: Mifuko ya Wakfu.
 - 3.8.5 Mitaji:
 - 3.8.6 Uwekezaji:
 - 3.8.7 Bodi za Wakurugenzi, viongozi watendaji na Wafanyakazi
 - 3.8.8 Ubia (*Partnerships*)
 - 3.8.9 Msaada wa kitaalamu (*Technical support*)
 - 3.8.10 Tabia na Maadili ya Kazi
 - 3.8.11 Kuleta Mabadiliko
 - 3.8.12 Masoko
 - 3.8.13 Kufungamana na Taratibu za Kishariah (*Shari'ah Compliance*)
 - 3.8.14 Utawala Bora
- 3.9 Mambo Muhimu Katika Kuleta Mabadiliko

- 3.9.1 Uchambuzi wa Hali Halisi (*Situation Analysis*)
- 3.9.2 Kushughulikia Mahitaji ya Jamii.
- 3.9.3 Matumizi ya Quran na Hadithi
- 3.9.4 Historia ya Kiislamu
- 3.9.5 Kutaja Mifano Bora ya Kuigwa
- 3.9.6 Kuvutia Wafadhili
- 3.9.7 Miradi ya Kiibada:
- 3.9.8 Ukarimu na Nia Njema
- 3.9.9 Wakfu ni Mtaji
- 3.9.10 Kuonekana na Kuweka Kumbukumbu Nzuri
- 3.10 Nafasi ya Wakfu Katika Kupunguza Umasikini
- 3.11 Nafasi ya Wakfu katika kukuza Ujasiriamali.
- 3.12 Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Teknohama) katika Wakfu
- 3.13 Wakfu wa Muda Maalum
- 3.14 Utaratibu wa Wakfu Zisizohamishika
- 3.15 Wakfu Wa Fedha Taslim (*Cash Waqf*)
- 3.16 Uwekaji Wakfu Kupitia Makampuni ya Bima Kiislamu (Takaaful)
- 3.17 Wakfu wa Miliki za Ubunifu (*Intellectual Properties*)
- 3.18 Usimamia wa Ardhi za Wakfu
 - 3.18.1 Njia za Kisheria
 - 3.18.2 Njia za Kiutendaji
 - 3.18.3 Njia za Matumizi
- 3.19 Usimamizi wa Nyumba za Wakfu
 - 3.19.1 Njia za Kisheria
 - 3.19.2 Njia za Kiutendaji
- 3.20 Kuchagua Taasisi Inayofaa Kuipatia Fedha Miradi ya Kuendeleza Mali ya Wakfu

**SURA YA NNE: UENDESHAJI WA MALI ZA WAKFU NA AMANA
(Kwa Mujibu Wa Sheria Namba 2 Ya 2007)**

- 4.1 Uwezo wa kusimamia Mali za Wakfu
- 4.2 Kufanya Wakfu Binafsi
- 4.3 Utenguzi wa Baadhi ya Wakfu
- 4.4 Usajili wa Wakfu Binafsi
- 4.5 Uwezo wa Kutaka Mahesabu Yanayohusiana na Mali ya Wakfu
- 4.6 Kuchukua Udhibiti wa Mali ya Wakfu katika Mazingira Maalumu
- 4.7 Uendeshaji wa Mali za Wakfu
- 4.8 Kuza Mali za Wakfu katika hali maalum
- 4.9 Uchukuwaji wa Mali za Wakfu
- 4.10 Usitishaji wa Muda wa Mikataba ya Ukodishaji
- 4.11 Kuongezwa Mikataba Mipyä ya Ukodishaji
- 4.12 Muda wa Kukodisha Mali ya Wakfu

- 4:13 Utumiaji Mbaya wa Mali ya Wakfu na Amana
- 4.14 Uendeshaji wa Wakfu unaofanywa na Mtu Binafsi
- 4.15 Mali ya Amana na Sadaka
- 4.16 Misikiti na Madrasa

REJEA

SURA YA KWANZA UTANGULIZI NA USULI

1.1 Maana ya Wakfu

Wakfu ni neno lenye asili ya kiarabu, na maana yake kilugha ni kuzuulia, kushikilia, kufungia au kusimamisha. Katika istilahi ya sheria ya Kiislamu lina maana ya kuhifadhi, kuzuulia au kufunga asili ya mali (kitu) katika dhima ya Mwenyezi Mungu (ili kisimiliwi na mtu mwengine) na kutoa Sadaka manufaa yake kwa lengo la kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Wakfu ni katika sadaka yenye kuendelea (*sadakatul jaariya*) ambayo muwekaji huwa ananufaika katika maisha yake ya dunia na akhera.

Mali ya Wakfu inaweza kuwa inayohamishika au isiyohamishika. Mali isiyohamishika inakusanya ardhi, majengo, miti, nyumba za makaazi na vitu vyengine visivyo hamishika vinavyofanana na hivyo na kukubalika kisheria. Ama mali inayohamishika inakusanya pesa, madini yenye thamani, hisa (*stock*), hati za kibenki (*bonds*), gari, haki za ubunifu (*intellectual right*), haki ya kukodi na vitu vyenginevyo vinavyohamishika vinavyokubalika kisheria. Mali inayotolewa Wakfu hairuhusiwi kuuzwa, kurithiwa, kugaiwa wala kutolewa zawadi.

Uwekaji wa Wakfu upo katika dini zote. Hata hivyo Uislamu uliondosha mapungufu yaliyokuwepo na kufanya maboresho katika mambo yafuatayo:-

- Ulikuza upeo wa malengo.
- Uliweka usimamizi wa kijamii.
- Uliweka kuwa ni wa maslahi ya Umma .
- Umeweka Wakfu wa kifamilia(kwa malengo mema).
- Umeweka uhifadhi mkubwa kwa njia mbili:-
 - Kupata kinga kwa kuwekwa katika umiliki wa Mwenyezi Mungu.
 - Matakwa yake kufuatwa kikamilifu kama nukuu (*naswi*) ya kisheria.

1.2 Malengo ya Wakfu

Uwekaji wa Wakfu unalenga kuleta maendeleo ya jamii kwa kuwasaiadia wahitaji, kuweka sawa maisha ya walio katika mazingira magumu, kunyanya viwango vya elimu, kuendeleza vipato vya watu, kusimamia nyumba na taasisi za ibada, misikiti, makaburi, hospitali, vituo vya ustawi wa jamii na kadhalika. Kwa upande mwengine Wakfu unaisafisha nafsi ya mwanadamu kutokana na ubinafsi na kupelekea kupendana. Nidhamu ya Wakfu inashajiisha kusaidiana, kuhurumiana na kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza umasikini na kuendeleza maisha ya watu na harakati za kijamii.

Wakfu ni katika mambo ya sunna yanayomkurubisha mja kwa Allah (S.W). Kuchukua sehemu ya manufaa ya kimali na kuwapa watu wanaostahiki ni katika amali zinazohimizwa na uislamu. Hivyo, Waislamu wanasisitizwa kujiwekea sadaka ambayo itakuwa inawanufaisha hata baada ya kuondoka duniani. Sadaka hizi zinaweza kuwa ni za kidini moja kwa moja mfano kujenga msikiti au inaweza kuwa ya kijamii mfano kujenga sehemu ya mapumziko kwa wasafiri au wapita njia. Moja ya sifa kuu za Wakfu ni kufungamana na lengo muhimu la kutenda wema.

Wakfu siku zote hubaki kuwa ni mtaji, na mapato yake ndio hutumika. Hivyo unakuwa ni sawa na mti wa matunda ambao kila mwaka unazidi ukubwa wake, unatoa matunda mengi zaidi na kuwanufisha watu wengi zaidi. Kwa msingi huu, hakuna sahaba yoyote wa Mtume (SAW) ambae alimiliki mali ila aliiweka Wakfu sehemu ya mali yake.

1.3 Historia ya Wakfu

Iwapo utapitia historia ya Wakfu kuanzia maandiko ya Sheria itakubainikia kuwa istilahi ya Wakfu kwa mara ya kwanza itumika katika sheria ya Mtume Muhammad (SAW) na haikuwa ikitumika zamani wala katika zama za Ujahilia. Katika hadithi za mwanzo mara nyingi Wakfu ilikuwa ikitajwa kwa jina la *Sadakatul Jaariya*.

Pamoja na kuwa halikuwa likitumika neno la Wakfu, lakini utekelezaji wake tunaukuta katika sheria zilizotangulia na katika jamii mbali mbali za ulimwengu. Mfano Mtume Ibrahim (A.S) alijenga Msikiti Mtukufu wa Makka na Masjidi Aqsa wa Palestina ambayo ilikuwa ni Wakfu na matumizi yake yalikuwa sawa kwa wakaazi wa miji hiyo na mingineyo. Aidha kisima cha maji ya zamzam kilikuwa Wakfu kwa Mahujaji, watu wa Makka na wapita njia. Tukiangalia sehemu nyingi za ibada za dini, jamii na miji tofauti tutazikuta kuwa zimebekwa Wakfu.

Katika historia ya Uislamu, kumbukumbu za Wakfu zinaanzia siku ya kwanza aliyofika Mtume (SAW) katika mji wa Madina. Baada ya kufika tu alianzisha Masjid Quba na baadee Masjid Nabawi. Vile vile imethibiti kuwa Mtume (SAW) aliweka bustani zake kuwa ni Wakfu, Sayyidna Omar (RA) aliliweka Wakfu shamba lake lililokuwa katika mji wa Khaibar, Sayyidna Othman (RA) alikinunua na kukiweka Wakfu kisima cha Ruma na hadithi ya Abu Talha kuweka Wakfu bustani aliyokuwa akiipenda zaidi ni maarufu. Aidha Malkia Zubeida mke wa Khalifa Haroun Rashiid alichimba visima vingi katika njia ya hijja na kuviweka Wakfu.

Historia ya Wakfu inaonesha mafanikio makubwa yalipatikana kuitia amali hii katika kuwasaidia watu masikini na kuendeleza ustawi wa jamii kwa ujumla. Aina mbalimbali za Wakfu zilianzishwa ili kuinufaisha jamii zikiwemo huduma za kijamii, elimu, tafiti na huduma za afya. Wanufaika wakubwa wa Wakfu walikuwa ni jamii kwa ujumla na kuwashirikisha masikini, wahitaji, mayatima, watu waliofungwa na familia zao.

Kulikuwa na nyakfu maalumu zilizohudumia kufanyika kwa tafiti za kisayansi kama vile elimu ya viungo vya mwili (*physiology*), elimu ya madawa (*pharmacology*), hesabu na elimu ya maumbile (*astronomy*). Wapo wataalamu na waandishi waliosema kuwa shughuli za kielimu na taaluma katika miji ya Kiislamu zilikuwa zikifadhiliwa kupitia Wakfu tu. Katika kuendeleza elimu, Wakfu zilijikita zaidi katika utoaji wa huduma za maktaba, vifaa vya kuandikia, mishahara ya walimu na wafanyakazi wengineo, dakhilia na huduma za kujikimu kwa wanafunzi. Tokea mwanzoni ufadhili haukuwa kwa masomo ya dini tu, bali ulihusu masomo yote. Aidha haukuchagua daraja wala uwezo wa watu na ndio maana tukawakuta wataalamu wakubwa waliotoka katika familia maskini sana. Elimu ya ufundi na amali pia ilipewa kipaumbele kutokana na umuhimu wake katika jamii.

Huduma za hospitali, utabibu na utoaji wa madawa zilikuwa ni moja ya sehemu muhimu zilizoshughulikiwa na Wakfu. Hospitali na vituo vingi vya Afya vilikuwa ni mali za Wakfu na zilihudumiwa kwa mapato ya Wakfu. Mnamo mwaka 1898 katika mji wa Istambul ilianzishwa Hospitali maarufu ya Shishli kwa ajili ya watoto kwa njia ya Wakfu.

Shughuli za kilimo pia zilipewa umuhimu mkubwa katika Wakfu. Yapo mashamba ya Wakfu ambayo yaliasisiwa kwa ajili ya kutoa mbegu bora au mapato yake kutoa mikopo ya mitaji na pembejeo kwa ajili ya kuendeleza kilimo. Katika baadhi ya nchi za Kiislamu ardhi za Wakfu zilifikia thuluthi moja (1/3) na zaidi ya ardhi yote ya kilimo na uwekezaji. Katika upimaji (*survey*) wa kwanza wa ardhi nchini Misri ambao ulifanyika wakati wa utawala wa Muhammad Ali ulionesha kuwa ekari 600,000 kati ya ekari milioni 2.5 za ardhi iliyotumika kwa kilimo zilikuwa ni Wakfu. Nyingi ya ardhi hizo zilikuwa ni za misikiti na huduma za kielimu na sehemu kubwa zaidi ilikuwa ni kwa ajili ya Chuo cha al-Azhar. Chuo Kikuu cha Al Azhar kilianzishwa Cairo mwaka 972 na kilikuwa kinahudumiwa kwa mali za Wakfu kwa kila kitu mpaka Serikali ya Misri ilipokichukua katika mwaka 1812 wakati wa utawala wa Muhammad Ali.

Serikali pia zilikuwa zikitekeleza baadhi ya majukumu yake kupitia Wakfu hususan katika sekta za elimu, afya, kilimo cha umwagiliaji maji, ustawi wa jamii, ulinzi na shughuli za kidini zikiwemo huduma za misikiti; madrasa na mishahara kwa ajili ya maimamu, walimu wa dini na wahadhi. Kwa kuzingatia kuwa elimu kwa ujumla wake ilichukua sehemu ya pili kwa kutumia mapato ya Wakfu, baadhi ya tawala ziliziwekea Wakfu maalumu skuli na vyuo ilivyovijenga. Mfano mzuri ni katika zama za tawala za Kiayubi (*Ayubites*) (1171-1249) na *Mamalik* (1249-1517) katika miji ya Misri na Palestina. Kumbukumbu zinaonesha kuwa mwanzoni mwa karne ya 20 Jerusalem ilikuwa na vyuo 64 vya fani mbali mbali ambavyo vilikuwa vikiendeshwa kwa Wakfu zilizomo Palestina, Uturuki na Syria. Vyuo 40 kati ya hivyo vilianzishwa na watawala na magavana wa Kiayubi na Kimamaliki.

Wakfu pia ulitumika katika kuwarahisishia watu safari za kuhiji Makka, kuwasaidia watu waweze kuoa au kuolewa na kuwashudumia wanawake wajane. Si hayo tu bali hata wapo

wanyama waliokuwa ni wanufaika wa Wakfu na wakati mwengine ultumika kupunguza wanyama waharibifu.

1.4 Historia ya Wakfu Zanzibar

Historia ya Wakfu Zanzibar inarejea tokea ujio wa Uislamu katika visiwa hivi. Katika kila zama mali zilizowekwa Wakfu na makusudio yake yaliendana na mahitaji ya kila wakati. Mwanzoni malengo makubwa ya Wakfu kwa Zanzibar yalihusu zaidi kuhudumia familia, malengo ya kiibada yakiwemo kusoma khitma, kuhiji, kufutarisha, kuhudumia masikini na mayatima, kuendesha miskiti na taasisi za kielimu. Kwa msingi huu mfumo wa Wakfu ultambulika rasmi kuwa ni utaratibu wa kisheria ulioruhusu kuweka mali kwa ajili ya kusaidia ustawi wa jamii na shughuli za kijamii na za kidini.

Historia ya Wakfu inaonesha kuwa hakukuwa na msikiti wowote uliojengwa hapa Zanzibar ila uliwekewa Wakfu wa kuuhudumia na kuendeleza. Baadhi ya misikiti pia iliwekewa Wakfu za kuendeleza darsa zilizoendeshwa au/na wanafunzi wanaosoma. Mfano mzuri ni Ukutani ambapo palikuwa na Wakfu nyingi zilizohudumia misikiti, vyuo pamoja na makaazi na huduma za kujikimu kwa wanafunzi waliotoka kila pembe ya visiwa vya Unguja na Pemba, Afrika ya Mashariki, Kati na Kusini. Kulikwa na nyumba maalumu za Wakfu kwa ajili ya wageni waliozuru Zanzibar, waliokatikiwa na njia, kutunza na kuhudumia wajane, mayatima, wagonjwa hasa wa maradhi ya muda mrefu na wenye haja nje na ndani ya Zanzibar.

Tunaweza kugawa mfumo wa maendeleo ya kiutawala ya Wakfu katika hatua nne zifuatazo:-

1.4.1 Usimamizi wa Wakfu Wakati wa Sultani (1832 – 1890)

Mnamo mwaka 1832 A.D Seyyid Said bin Sultan alihamisha rasmi makao yake kutoka Oman kuja Zanzibar. Wakati wa utawala wa Kisultani, wanachuoni (maulamaa) walihesabika kuwa ni katika kundi la wataalamu na walikuwa na hadhi na nafasi kubwa katika Mahkama na utawala wa Sultani. Maulamaa walikuwa na ushawishi mkubwa katika sera na maamuzi ya Sultani. Katika kipindi hiki, uangalizi wa Wakfu ulikuwa unafanya chini ya Waziri wa Wakfu. Mara nyingi nafasi hii alikuwa akiteuliwa mtu anayeheshimika mionganoni mwa masheikh wakubwa wa Zanzibar na aliyepata imani ya kiutendaji kutoka kwa Sultani. Lengo kuu la Wakfu kwa wakati huu lilikuwa ni kuhifadhi, kulinda na kuendeleza mali na haki za Jumuiya za Kiislamu, kuendeleza shughuli za kidini, kiutamaduni kijamii na kielimu. Pia ililenga kupunguza umasikini katika jamii ya Kizanzibari na Kiislamu kwa ujumla.

1.4.2 Usimamizi wa Wakfu Wakati wa Waingereza (1890-1963)

Baada ya kifo cha Sultan Hamoud bin Mohammed (1896-1902), Mwanamfalme Ali bin Hamoud (1902-11) aliyekuwa chini ya umri wa miaka 14 aliteuliwa na utawala wa Kiingereza kuwa

Sultani wa Zanzibar. Hii ilikuwa ni fursa kwa Balozi Mkaazi wa Kiingereza aliyekuwa Zanzibar Bw. Rogers kuwa na mamlaka kamili ya kiutawala akiwa kama ni Waziri Mkuu na Kaimu wa Sayyid Ali bin Hamoud hadi alipofikia umri wa utuuzima wa miaka 18 katika mwezi wa Juni 1905. Mara Bw. Rogers alipochukua mamlaka kamili ya kuitawala Zanzibar kwa takriban miaka mitatu hivi, aliweza kufanya mabadiliko makubwa ikiwemo kuweka utaratibu mwengine wa hazina ya Kiislamu (*Bait ul Maal*). Mapato mengi ambayo Sultani alikuwa akiyatuma kwa ajili ya kusaidia masikini, watu wahitaji na kuunda baadhi ya miundo mbinu ya Zanzibar iliwekewa taratibu nyengine ikiwemo kutumika katika mipango mbali mbali ya kiserikali.

Sheria ya awali ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ilianzishwa mnamo mwaka 1905. Aidha utawala wa Kiingereza uliweka taratibu zilizohakikisha kuwa mali zote za Wakfu, urithi na zinazotolewa kwa shughuli za Kiislamu zinaratibiwa na kusajiliwa kiserikali. Kuanzia kipindi hiki ambacho Sultani alipoteza nguvu nyingi za kiutawala hadi mwaka 1963 ziliwekwa sheria na kanuni nyingi zilizohakikisha kuwa Waingereza wanaidhibiti kikamilifu Kamisheni ya Wakfu. Sheria za Wakfu zilimpa mamlaka Balozi Mkaazi wa Kiingereza kuchagua Makamishna wa Wakfu na kupeleka majina yao kwa Sultani ambae kiheshima tu aliwateua na kuwatangaza rasmi. Mara nyingi makamishna wengi zaidi walikuwa si waislamu na hata uteuzi wa watendaji wakuu wa Kamisheni haukuzingatia dini.

Katika kipindi hiki sheria ya Wakfu, muundo na utaratibu wa kiutawala ulikuwa ukibadilishwa mara kwa mara kwa kuzingatia mahitaji na changamoto zilizojitokeza. Kati ya mabadiliko na masahihisho hayo ni *Waqt Decree no. 2 ya 1905; Decree mpya ya Wakfu no. 2 ya 1907; Waqt Decree no. 15 ya 1909 (amendment); Waqt Property Decree no. 16 ya 1916 ; Waqt Validating Decree no. 5 ya 1946; Waqt Validating Decree no. 6 ya 1951 (amendment); na Waqt Property Decree ya 1959 Cap. 103 ya sheria za Zanzibar.*

Pamoja na kuteuliwa viongozi walioridhiwa na utawala lakini shughuli za Wakfu hazikuwa nyepesi. Baadhi ya wakati Waingereza waliingilia kati kuamrisha baadhi ya mambo ambayo mengine yalikuwa ni kinyume na taratibu za kidini na hata sheria zilizokuwepo. Wakati mwengine viongozi hao walipata vitisho vya kuzuwiwa maposhio yao au kuondolewa katika Ukamishna. Wapo waliojiuzulu nyadhifa zao kwa kutokukubali kuendana na sera au maagizo waliyopewa.

Miongoni mwa mambo muhimu yanayopatikana katika kipindi hiki ni usajili wa mali na milki nyingi za Wakfu hasa mashamba na ardhi, misikiti iliyojengwa ilikuwa ikiwekewa Wakfu wa kuihudumia, Wakfu za Kijamii (kikabilo) na kimadhehebu zilikuwa na nguvu na kulikuwa na mali za Wakfu nje ya nchi zilizonufaisha Wazanzibari au Zanzibar zikanufaisha nje ya nchi hususan katika nchi za kiislamu kama vile Oman, Makka, Madina na Uturuki.

1.4.3 Usimamizi wa Wakfu Kuanzia Mapinduzi ya 1964 hadi 2007

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya mabadiliko ya usimamizi wa Wakfu tokea siku za awali ili kudhibiti mali za Wakfu. Muundo wa usimamizi ulibadilika kwa kuzichanganya shughuli za Wakfu na Mali za Amana katika Ofisi ya Kabidhi Wasii (*Administrator General*). Sheria nyingi zilitungwa zikiwemo *Waqt Property Decree* ya 1965 (*amendment*), *Presidential Decree no. 12 ya 1965, Presidential Decree no. 12 ya 1966* na *Waqt Property Decree* no. 7 ya 1967 ambayo ilifuta vifungu vingi vya *Waqt Property Decree and Public Trustee Decree, Cap. 24*.

Kipindi cha awali cha awamu hii kilishuhudia kutelekezwa kwa mali na haki nyingi za Wakfu, kutopatiwa matunzo, kutotekelizwa wasia na nyengine kupotea. Nyaraka na kumbukumbu nyingi ziliparaganyika. Aidha kwa kuzingatia sera zilizokuwepo Wakfu za Jumuiya za kijamii na kimadhehebu zilidhoofika sana na uhusiano wote na nyakfu zilizo nje ya nchi ulikatika. Baadhi ya Wasimamizi wa Wakfu walilalamikia sheria iliyotaifisha mashamba mengi ya Wakfu na kuyagawa eka tatu tatu kwa wananchi na amri iliyozitaka Jumuiya zote za Kijamii kukabidhi milki zote za Wakfu kwa Msimamizi wa Mali za Wakfu. Baadhi ya Maimamu walilalama kuwa misikiti yao imekuwa katika hali mbaya kwa sababu hawakuwa wakipata mapato ya mali zilizowekewa misikiti hiyo na hawakuwa na mamlaka ya usimamizi wa mali hizo uliokuwa kwa Kamisheni. Uwekaji wa Wakfu kwa mali mpya ulizorota sana katika kipindi hiki.

Shughuli za Usimamizi wa Wakfu ziliendelea hivyo mpaka mwaka 1980 ambapo Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ilianzishwa upya kwa Dikrii namba 5 ya Baraza la Mapinduzi. Kuanzishwa upya kwa Kamisheni kulilenga pia kuratibu shughuli za Kiislamu zikiwemo Zaka, Sadaka, Hijja, Sala na Mabaraza ya iddi na nyenginezo ambazo pia zilisimamiwa na Serikali. Muundo wa Kamisheni ulibadilika ambapo Kadhi Mkuu alikuwa ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Kamisheni na kuliwekwa makamishna wasiozidi sita amba waliteuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mionganoni mwa viongozi wa Kiislamu, maulamaa na masheikhe. Katibu Mtendaji ambae pia anateuliwa na Rais ndiye Mtendaji Mkuu wa shughuli za kila siku za Kamisheni. Katika mwaka 2001 yalifanyika marekebisho kuititia Sheria ya Mufti ambayo ilimuweka Mufti wa Zanzibar kuwa Mwenyekiti wa Kamisheni badala ya Kadhi Mkuu, aidha ilibadili utaratibu wa kuteua wajumbe wa Bodi na kupewa jukumu hilo Waziri anaehusika na sheria ya Kamisheni badala ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Katika kipindi hiki cha mwisho juhudu kubwa ilichukuliwa ya kuzirejesha mali za Wakfu na Amana katika usimamizi wa Kamisheni. Mafanikio makubwa yalipatikana kwa upande wa nyumba hususan zilizopo katika eneo la Mji Mkongwe. Hata hivyo, uchakavu wa nyumba hizo na kukosekana kwa kumbukumbu za kutekelezwa Wakfu husika ilikuwa ni changamoto kubwa. Aidha zipo mali zilizouzwa zikiwemo za Pemba na mapato yake kuchanganywa na kujengwa nyumba za pamoa Unguja lakini bado baadhi ya kumbukumbu zake hazijulikani.

Mnamo mwaka 1977 Rais wa Zanzibar aliwakusanya masheikhe na wanachuoni kwa kuwashauri na hatimae akaunda tume ya kutathmini milki za Wakfu zilizotaifishwa na kutumika

kwa shughuli za umma au kukatwa eka na kugawiwa wananchi. Masheikh walitakiwa watowe uamuzi wa Kisheria ima milki hizo warejeshewe wenyewe au yalipwe fidia kwa thamani yake pamoja na ghila la miaka 13 kuanzia 1964 hadi 1977, muda ambao hayakuwa yakitoa tija kwa nyakfu husika. Masheikhe waliama mashamba hayo yalipiwe fidia na Ripoti ya Tume ilitathmini jumla ya shillingi 52,744,745 zilipwe zikiwa ni thamani ya mashamba na shilingi 49,709, 166 zikiwa ni badala ya ghila. Awali Serikali iliahidi kulipa shillingi 2,000,000 kila mwezi, lakini baadae ikasita. Hata hivyo, fedha zote hizo zimeshalipwa. Kamisheni imeziwekeza fedha zote hizo katika mradi wa nyumba zilizoko Mbweni na wanufaika ni mashamba yote husika.

Pamoja na jitihada hizo, ilibainika kuwepo kwa mashamba mengi ambayo bado hayakulipwa fidia. Mfano viunga vya wakfu za Muhera binti Juma Jang'ombe, Moza binti Saidi Saateni, na Omar Said Salim Chumbuni vilivyojengwa nyumba. Aidha kulikuwa na nyumba zilizovunjwa kwa kazi za kitaifa bila kulipwa mfano Wakfu wa Jenabai na wa Msikitii Hanafi Mtemani Wete, Wakfu wa Saleh Lalji wa Kichungwani. Aidha kulikuwepo nyumba za Amana za mayatima ambazo zilihodhiwa kwa namna tofauti. Hali hii ilipelekea Baraza la Mapinduzi mnamo mwaka 1993 kutoa agizo la kulipwa fidia mashamba ya Wakfu yaliyokatwa eka, na pia liliagiza mashamba na milki zote ya Wakfu na ya Mayatima (Amana) ambazo zilikatwa eka na/au ziko mikononi mwa taasisi za Serikali zirejeshwe katika dhamana ya Kamisheni na mashamba yaliyogawiwa kwa wananchi pale watakafariki waliokabidhiwa pia yakabidhiwe Kamisheni. Utekelezaji wa agizo hili ulipewa tafsiri tofauti katika ngazi za utendaji na hivyo kusababisha kutokutekelezeka vyema. Hali hii pia ilipelekea ufujaji wa mali nyingi za Wakfu na mashamba mengi yenye rutba yaliyo karibu na miji kukatwa viwanja.

1.4.4 Usimamizi wa Wakfu Kuanzia 2007 hadi Sasa

Kamisheni iliundwa upya kwa sheria namba 2 ya mwaka 2007. Kwa mujibu wa sheria hii Kamisheni ni taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye hadhi ya kujitegemea, ikiwa na muhuri na nembo yake. Kamisheni ina uwezo wa kuendesha, kuratibu, na kupanga kwa kutumia jina lake jambo lolote lililomo katika mamlaka yake kwa mujibu wa masharti ya Sheria hiyo, Sheria za Kiislamu, kanuni na maadili mema. Aidha, kwa jina lake Kamisheni ina uwezo wa kushtaki na kushtakiwa; kupata, kununua na kugawa au kutumia mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika na kuingia katika mkataba kwa madhumuni yoyote ambayo ina uwezo nayo.

Kuna Bodi ya Uongozi ya Kamisheni yenye Mwenyekiti anayeteuliwa na Rais, Katibu Mtendaji anayeingia kwa nafasi yake na wajumbe wengine wasiopungua watatu na wasiozidi watano wanaoteuliwa na Waziri kwa kuzingatia sifa mbali mbali zenyenye uhusiano na kazi za Kamisheni.

Kazi kuu za Kamisheni kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

- Kusimamia mali za Wakfu; mali za Amana na mali (tirka) za marehemu waislamu.
- Kuratibu shughuli za Hijja.
- Kuratibu na kupanga shughuli za kukusanya na kugawa Zaka, Sadaka na Misaada ya kheri.

- Kuratibu Sala na Mabaraza ya Iddi kitaifa.

Sheria ya Kamisheni namba 2 ya 2007 imechambua kwa upana utendaji wa kila kazi na kuweka mazingira mazuri ya kufanikisha majukumu ya Kamisheni kwa mujibu wa mahitaji ya zama zilizopo. Pia imetoa nafasi ya kutungwa Kanuni na kutolewa Miongozo kwa usimamizi mzuri wa kazi hizo.

Kamisheni imepiga hatua kubwa katika kuimarisha utendaji wake. Kati ya Mafanikio yaliyopatikana ni:-

- Kuzidisha ufanisi katika usimamizi, uhifadhi na uendelezaji wa mali za Wakfu na Amana.
- Kuimarisha taratibu za mirathi na kuhakikisha uadilifu katika ugawaji wa haki.
- Kuanzisha nidhamu ya Zakka na kusaidia katika uwezeshaji wananchi kiuchumi.
- Kuboresha huduma na ufanisi katika taratibu na shughuli za Hijja.
- Kufanikisha Sala na Mabaraza ya Iddi kwa kuzingatia mahitaji ya kidini na zama.
- Kukuza uelewa wa Mafunzo ya dini ya Kiislamu kwa ujumla na kazi za Kamisheni kwa khususi.
- Kuimarisha uhusiano na taasisi za nje na ndani ya nchi zenyenye malengo yanayofanana.
- Kuanza taratibu za uhifadhi wa kumbukumbu na utoaji wa huduma kwa mfumo wa kielektronia.

1.5 Makusudio ya Muongozo

Makusudio ya Muongozo huu ni kuweka dira na kuwajengea uwezo wadau wote wa Wakfu ili waweze kutekeleza sheria na taratibu za Wakfu wakiwa na uelewa wa kutosha ili nidhamu ya Wakfu iweze kutoa matunda yaliyokusudiwa. Kwa kuzingatia msingi wa kisheria usemao “*Haikatazwi kubadilika baadhi ya ahkami kwa kubadilika zama*” Muongozo huu umelenga kuunda nidhamu ya Wakfu kwa kuzingatia mahitaji na maendeleo ya wakati tulionao. Ahkam nyingi za Wakfu zimethibiti kwa njia za Ijtihadi, hivyo bado wanachuoni wanaendelea kujitahidi na kupelekea maendeleo na mageuzi mengi katika uwekaji, usimamizi, uendelezaji na unufaikaji katika Wakfu.

SURA YA PILI

MAELEZO YA WAKFU NA MISINGI YAKE

2.1 Asili ya Sheria za Wakfu

Zipo aya za Kurani zinazoonesha maana ya Wakfu kwa ujumla wake tu mfano Mwenyezi Mungu aliposema: (*((Hamtoweza kuufikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda; na chochote mnachokitoa, basi kwa hakika Mwenyezi Mungu anakijua))*). Aali Imran: 92. Pia amesema :((*Enyi mliaoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikia (kufikia Pepo yake) na fanyeni juhudhi kwa ajili ya dini ili mpage kufaulu*)). Al Maida: 35.

Wanachuoni walio wengi wanasema asili ya sheria za Wakfu ni Sunna za Mtume (S.A.W) na *ijmaa* ya wanachuoni. Ama kwa upande wa Sunna ni hadithi iliyothibiti kuwa hakika Omar RA alisema: *Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hakika mimi nimepata mali katika ardhi ya Khaibar na sijapatapo kamwe kupata mali yenyeye thamani zaidi kuliko hiyo. Jee unaniemuru niifanye nini? Akasema (SAW): "Ukipenda uizuwie asili yake na uitolee sadaka (manufaa) yake isipokuwa haitauzwa asili yake wala haitatolewa zawadi wala haitarithiwa."* (Imepokewa na Ahmad, Bukhari, Muslim, Tirmidhy, Nasai, Abu Daud na Ibnu Majah).

Kwa msingi huo Sayyidna Omar R.A aliiweka Wakfu mali kwa kunufaisha mafukara, jamaa zake, kukomboa watumwa, kutumika katika njia ya Mwenyezi Mungu na kwa waliokatikiwa na njia. Pia akaruhusu atakayeisimamia kula katika mali hiyo kwa namna inayokubalika au kumlisha rafiki yake. Pia imepokewa kutoka kwa Bukhari na Muslim kuwa Mtume (SAW) Amesema: *"Anapokufa mwanadamu amali zake hukatika ila kwa mambo matatu. Sadaka inayoendelea, au elimu inayonufaisha au mtoto mwema anayemuombea dua."* Sadaka inayoendelea katika hadithi hii imetafsiriwa kuwa ni Wakfu. Imepokewa pia kuwa Mtume SAW mwenyewe aliweka Wakfu wa mashamba yake kwa ajili ya Bani AbdulMutwalib. Pia imethibiti kuwa hakukuwa na sahaba yejote wa Mtume (SAW) ambae alikuwa na mali ila aliweka Wakfu.

Imam Nawawi na Ibn Qudama wameeleza kuwa wanachuoni wamekubaliana kuhusiana na kuwepo kwa sheria ya Wakfu na kulifanya jambo kuwa ni *Ijmaa*.

2.2 Hekma za Kuletwa Sharia ya Wakfu

Kuna hekma nydingi zinazopatikana katika sheria ya Wakfu. Kati ya hekma hizo ni:-

- a) Kuwawezesha waja kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa mali zao hasa wale ambao Mwenyezi Mungu amewapa wasaa katika mali.
- b) Kutoa nafasi ya mja kunufaika na mali yake baada ya kifo chake.

- c) Kutoa fursa kwa mja kuendelea kuwanufaisha kwa mali yake anaowapenda wakiwemo jamaa, masikini na shughuli za kheri katika jamii.
- d) Ni sababu kubwa ya kujenga, kuendeleza na kuimarisha taasisi za kidini, kijamii na shughuli za kiibada, kiuchumi na kimaendeleo.

2.3 Aina za Wakfu

Wakfu zinagawiwa kwa kuzingatia wanufaika katika aina mbili kuu. Mazingatio katika mgao huu ni ile aina ya mwanzo ya wanufaika waliowekewa mali husika ya Wakfu. Kwa msingi huo, Wakfu zipo kama ifuatavyo:-

- i. Wakfu wa kheri: Ni ule uliowekwa mwanzo kunufaisha mambo ya kheri mfano misikiti, madrasa, kusaidia masikini, kuendeleza shughuli za elimu au hospitali na kadhalika; hata kama baadae utawekwa kunufaisha jamaa wa muweka Wakfu.
- ii. Wakfu wa Jamaa: ni ule mtu anaojiwekea mwenyewe, mtu mwengine mwenye uhusiano nae, watu maalumu na hata kama mwisho utapelekwa katika mambo ya kheri. Mfano kunufaika mwenyewe, kisha watoto wake, kisha jambo la kheri.

2.4 Nguzo za Wakfu

Ili Wakfu ukamilike ni lazima zitimie nguzo nne kama zifuatazo:-

- i. Muwekaji Wakfu (*Waqif*) .Ni lazima awe baleghe, mwenye akili timamu na asiwe amelazimishwa.
- ii. Kitu au mali inayowekwa Wakfu (*Mawquf*). *Mawquf ni lazima kijulikane na kiweze kutumika*
- iii. Wanufaika wa mapato au mali za waqfu (*Mawquuf 'alaihi*).
- iv. Maneno ya kuweka Wakfu mali au kitu (*Sighah*).

2.5 Namna za Kuweka Wakfu

Kuweka Wakfu kunakuwa kwa lafdhi za mdomo zilizowazi au kimafumbo, maandishi au vitendo kama inavyoonekana katika ufanuzi ufuatao:.

- i. Ama lafdhi zilizo wazi ni kusema au kuandika nimeweka Wakfu, nimekifunga au nimekisabilia kitu fulani.
- ii. Maneno (lafdh) ya kimafumbo ni kusema au kuandika nimekitolea sadaka, nimekizuwia au nimekihifadhi milele kitu fulani. Lafdh za mafumbo zitakuwa ni Wakfu iwapo zitaambatana na walau moja kati ya mambo matatu yafuatayo:-
 - a. Nia ya kuweka Wakfu.
 - b. Kuandamana na lafdhi ya wazi mfano nimeitoa sadaka ya kuifunga, au ya kuisabilia au ya milele au ya kuizuwia.
 - c. Kukisifu kitu kwa sifa za Wakfu mfano kusema Sadaka hii ni haramu kuuzwa, wala kugaiwa wala kurithiwa.

- iii. Kwa kuzingatia kanuni ya kisheria isemayo “*kilichoandikwa ni sawa na kilichotamkwa*” hivyo yale yote yanayohusiana na maneno yatachukua hukmu ya Wakfu iwapo yataandikwa.
- iv. Wakfu wa vitendo ni kufanya ishara au kitendo kinachoonesha kuwa ni Wakfu mfano kujenga jengo kisha likaadhiiniwa ili kusaliwa au kuchimba kisima kisha ukawakabidhi wanajamii watumie.

Tanbihi: Pamoja na kuwa likifanyika moja kati hayo mali iliyowekwa Wakfu itakuwa ni Wakfu mbele ya Mwenyezi Mungu lakini Mweka Wakfu atapaswa kuzingatia taratibu nyengine za kisheria ikiwemo kusajili Wakfu huo katika Mamlaka husika ili uweze kupata kinga na haki nyengine za kisheria.

2.6. Wahusika wa Wakfu

Katika uendeshaji wa shughuli za Wakfu wapo wahusika wa aina tatu ambao wanahusiana moja kwa moja na mali ya Wakfu. Wahusika hao wenye majukumu na haki mbali mbali ni Muweka Wakfu, Msimamizi na Mnufaika. Maelezo kwa ujumla kwa kila mmoja ni kama ifuatavyo:-

2.6.1 Muweka Wakfu(*Waqif*)

Waqif ni mtu, watu au taasisi inayotoa mali na kuiweka Wakfu. Inawezekana mtu huyo kuweka Wakfu kwa ajili ya nafsi yake au kumuwekea mtu mwengine. Kwa mfano mtoto anaweza kuweka Wakfu ili thawabu azipate mzee wake lakini katika hali hiyo Waqif atahesabika kuwa ni huyo mtoto hata kama Wakfu utaitwa kwa jina la mzee wake. Kwa vile Waqif ndiye aliyeimiliki mali na kuiweka Wakfu makusudio yake na maelekezo yake aliyyoyatoa wakati anaweka Wakfu ni lazima yatekelezwe.

2.6.1.1 Sharti za Muweka Wakfu

Kuweka Wakfu ni jambo la hiari. Hata hivyo, yapo masharti maalumu yanayopaswa kuwepo ili kuufanya Wakfu uwe sahihi. Masharti hayo yatamhusu Waqif, mali inayowekwa Wakfu na utaratibu wa uwekaji Wakfu kama ifuatavyo:-

- a) Aimiliki mali anayoiweka Wakfu umiliki uliokamilika kisheria. Hivyo haifai kuiweka Wakfu mali aliyoipata kwa wizi, unyang'anyi, dhulma au hata aliyoinunua lakini akawa hajakabidhiwa rasmi.
- b) Awe ni mwenye akili timamu. Hivyo haisihi kwa mwendawazimu au aliyechanganyikiwa.
- c) Awe ni baleghe. Hivyo hausihi Wakfu wa mtoto hata kama ni mwenye kupambanua.
- d) Awe ni mwenye utambuzi kisheria. Hivyo hausihi Wakfu wa mtu aliyezuiliwa kufanya matumizi kisheria, aliyefilisiwa au aliyehafilika.
- e) Awe na nia ya dhati kwa kuweka Wakfu kwa hiari yake, sio kwa kulazimishwa.
- f) Malengo ya Wakfu yakubalike kisheria.

2.6.1.2 Haki za Muweka Wakfu

Kanuni ya kisheria inasema “*Shartul waaqif ka naswi Shaarii*” yaani masharti ya muweka Wakfu yana nguvu sawa na nukuu ya kishariah. Hivyo masharti yake ni lazima yatekelezwe madhali hayendi kinyume na shariah. Waqif ana haki ya kumuwekea Wakfu amtakae na anaweza kujiwekea ye ye mwenyewe, anaweza kumteua msimamizi au kuusimamia mwenyewe na anaweza kubainisha namna ya uendeshaji.

2.6.2 Msimamizi wa Wakfu (*Mutawalii*)

Muweka Wakfu anaweza akajiweka mwenyewe kuwa ndie msimamizi wa kwanza au hata mnufaika. Msimamizi anaweza kuwa mwanamme au mwanamke iwapo tu atakuwa na sifa zinazohitajika kwa *Mutawalii*. Vile vile kikundi cha Watu wakiwa kama kamati au taasisi wanaweza kupewa jukumu la usimamizi wa mali ya Wakfu.

Mutawalii atasimamia Wakfu kwa kuzingatia matakwa ya *Waqif* kuhusiana na wanufaika na namna ya uendelezaji wa mali za Wakfu. Hivyo ana wajibu wa kuichunga mali ya Wakfu, kuitunza, kuihifadhi na kuitekelezea yale yaliyokusudiwa kunufaisha. Kwa msingi huo *Mutawalii* ni lazima awe muadilifu na mwenye uwezo wa kusimamia mali za Wakfu. Ni lazima awe mbunifu ili aweze kuendana na wakati hasa ukizingatia kuwa mambo mengi ya Wakfu yamethibiti kwa kujitahidi hivyo huwa yanabadilika kwa kubadilika zama. Msingi wa kisheria unasema "*Haikatazwi kubadilika baadhi ya ahkami kwa kubadilika zama*".

Kwa mwelekeo wa siku hizi mara nyingi wasimamizi wa Wakfu huwa ni taasisi zilizosajiliwa rasmi. Ili taasisi ifae kusimamia Wakfu ni lazima itimize masharti yafuatayo:-

- a) Isiwe yenyelengo la kupata faida tu.
- b) Iwe inatambuliwa kwa kusajiliwa rasmi.
- c) Iwe inawezekana kuendelezwa.
- d) Iweze kufanya ushawishi wa kuleta mabadiliko ya kisheria kila hali inapolazimu.
- e) Iwe na uwezo wa kutunza kumbukumbu na nyaraka za nyakfu husika.
- f) Iwe na uwezo na uthubutu wa kuzilinda mali za Wakfu.

Iwapo *Mutawalii* ameshindwa kutekeleza wajibu wake au anakosea ni wajibu kwa muweka Wakfu, wanufaika, mamlaka zinazosimamia Wakfu au muislamu ye yote kumsawazisha. Ama ikithibiti kuwa ameshindwa kuusimamia au amekosa uadilifu basi mtu ye yote anaweza kuomba Mahkamani aondoshwe baada ya kuthibitisha dai lake.

2.6.2.1 Usimamizi wa Mali za Wakfu Kitaifa

Ilizoeleka kuwa mara nyingi Wakfu ulikuwa unasihamiwa na mmoja wa wanufaika au wanafamilia wa *Waqif*. Kutokana na mabadiliko ya zama na ili kuleta ufanisi katika usimamizi wa Wakfu mara nyingi hivi sasa mali za Wakfu zinasimamiwa na taasisi maalumu ima zinazofanya kazi nchi nzima, katika maeneo maalumu au hata katika jumuiya fulani. Taasisi inayosimamia mali za Wakfu kitaifa inahitajika kuwa na sifa zifuatazo:-

- i. Timu ya wataalamu weledi (*Corporate Professionalism*) katika majukumu yao.
- ii. Uwazi na uwajibikaji.
- iii. Kuwa na sheria, kanuni na miongozo madhubuti.
- iv. Ustadi na ubunifu katika mipango ya usimamizi, uhifadhi na uendelezaji.
- v. Uadilifu.

2.6.2.2 Uendelezaji Mali za Wakfu

Ili mali za Wakfu zilete tija na zidumu, zinahitaji kuendelezwa. Mwenye wajibu wa kuendeleza mali za Wakfu ni Msimamizi. Uendelezaji wa mali hizo utategemea hali na mahitaji na unaweza kuwa kwa:-

- i. Kuanzisha mitaji na miradi ya Wakfu.
- ii. Kuwekeza kwa kuiunganisha na miradi mingine ya kimali.

Katika kufanikisha haya kunahitajika uadilifu, ujuzi, stadi, sheria madhubuti na uwazi. Iwapo uendelezaji utakuwa mzuri mali ya Wakfu itakuwa nyingi zaidi na hivyo kutoa manufaa zaidi na thawabu nyingi zaidi kwa *Wakif*. Ibainike kuwa Wakfu pia unaweza ukawa na milki zake nje ya asili ya Wakfu. Mfano mtu atatoa mali kwa ajili ya kuongezea mtaji wa Wakfu, mali hiyo itakuwa ni milki ya Wakfu husika na sio Wakfu.

Miongoni mwa mambo muhimu pia kwa Msimamizi katika kuendesha mali za Wakfu ni:-

- Kuweka rikodi za Wakfu mmoja mmoja na zile za kitaifa
- Kuhifadhi na kuziendeza mali za Wakfu
- Kutumia mikataba iliyо madhubuti kwa kuzingatia urfu (desturi) na mahitaji ya zama.
- Kutenganisha baina ya muendeshaji na mmiliki.
- Kuziwekea mali za Wakfu heshma na kinga madhubuti kijamii.

2.6.3 Wanufaika wa Wakfu

Mnufaika wa Wakfu ni mtu au taasisi ambayo hupata manufaa ya mali ya Wakfu. Wanufaika wamegawika sehemu mbili. Wanufaika waliopo ambao ndio wenyе haki ya kunufaika na Wakfu na wanufaika watakao kuja ambao watapata uhalali wa kunufaika baada ya kuondoka wanufaika waliopo. Kwa mfano mtu akiwawekea Wakfu watoto wake kisha uhudumie msikiti, hivyo Wakfu hautahudumia msikiti mpaka watoto wote watakapofariki. Hivyo hivyo, iwapo atausia watoto, kisha wajukuu, hawatanufaika wajukuu mpaka watoto wote wamalizike.

Mnufaika aliyepo na watakaokuja baadae wote wana haki sawa. Hivyo, wanufaika hawana haki ya kuamua vyenginevyo kuhusu kubadilisha manufaa au wanufaika. Watakapohisi kuwa Wakfu hauleti tija iliyokusudiwa watalazimika kumjuulisha msimamizi, na iwapo wanaona msimamizi hafanyi haki pia basi watapeleka shauri lao mahakamani.

2.6.3.1 Aina za Wanufaika

Wanufaika wa Wakfu wanaweza kuwa ni familia, jamii au familia na jamii kwa pamoja. Ufafanuzi wa hayo unakuwa kama ifuatavyo:-

i). **Familia** inakusudiwa jamaa wote wa *Waqif* sawa kama ni kwa sababu ya nasabu mfano mtoto, mjukuu, baba, mama na ndugu; sababu ya ndoa mfano mke, mume, mkwe au shemegi; au hata mlezi au watoto wa kulea na familia zao. Katika Wakfu wa familia kwa ujumla wake, wanufaika wote wanapata sawasawa na wanaoingia ni watoto na watoto wa watoto wanaume. Kwa vile maelekezo ya *Waqif* ndio yanayofuatwa inabidi abainishe kwa uwazi kabisa kama watoto wote wapate sawa au wenye sifa gani wazidi; kama waingie watoto wa watoto wanaume tu au hata wa watoto wa watoto wanawake ; aidha abainishe unufaishe nini iwapo kizazi kitakatika.

Utafiti uliofanyika katika nchi nydingi duniani umebainisha kuwa kutokana na mabadiliko ya hali ya maisha utaratibu wa kuweka Wakfu nyumba au shamba kwa familia kizazi baada ya kizazi kwa sasa hauleti manufaa. Utaratibu huu unapelekea kutelekezwa Wakfu na hatimae kuangamia au kuhodhi manufaa hayo baadhi tu ya wanufaika na hivyo kusababisha dhulma. Kwa mfano mtu atawawekea Wakfu nyumba watoto wake wanne kisha wajukuu na kuendelea kizazi hadi kizazi. Hii ni kusema kuwa wanufaika wa nyumba hiyo watakuwa wanne kwa watoto, wajukuu wanaweza kuwa 16, kizazi kinachofuata ni 64 kisha 256. Hali hii iwapo kila mtoto atakuwa anapata watoto wanne tu. Kwa msingi huo inapendekezwa mtu anayependa kuweka Wakfu basi ni vyema akauweka kwa watoto wake tu au labda na wajukuu kisha unufaishe maslahi ya ujumla mfano nyumba za ibada, hospitali au makundi maalumu kama vile mayatima, wagonjwa, wanafunzi na mfano wa hayo.

ii). **Jamii** inakusudiwa jambo lolote la kheri ambalo litanufaisha baadhi ya wanajamii au jamii yote bila ya kuifunga na familia. Mfano kuwawekea Wakfu masikini, waumini, wagonjwa, wakaazi wa mji fulani, wanafunzi, taasisi au kundi lolote la kijamii linalokubalika katika sheria ya Kiislamu.

iii). **Familia na jamii** zinakusanya makundi mawili na yanaweza kwenda sambamba kwa wakati mmoja mfano mtu kuweka Wakfu kwa ajili ya watoto wake na wanafunzi au inaweza kunufaisha familia kisha jamii; au jamii kisha familia kisha jamii.

Tanbihi: Wanufaika wa Wakfu sio lazima kuwa Waislamu. Taasisi au mtu yejote anaweza kunufaika na Wakfu hata kama sio Muislamu madhali sio maadui wanaodhihirisha uadui wao kwa Uislamu. Ushahidi wa hayo ni kuridhiwa kwa Wakfu wa Bi Safia RA, mmoja wa wake wa Mtume SAW kwa ndugu zake waliokuwa katika dini ya Kiyahudi.

2.6.3.2 Namna ya Kunufaika na Wakfu

Mnufaika wa mali ya Wakfu anaweza kunufaika kwa Wakfu kwa kuutumia mwenyewe mfano kukaa katika nyumba, kujipamba kwa mapambo, kupanda kipando na kadhalika. Pia anaweza kunufaika kwa kodi, mapato au haki zitakazopatikana baada ya mali ya Wakfu kupangishwa kwa watu wengine.

2.7 Kilichowekwa Wakfu (Mawquuf)

Makusudio ya kilichowekwa Wakfu ni mali au haki sawa kama inahamishika au isiyohamishika ambayo imewekwa katika dhima ya Allah(S.W) na kutolewa sadaka manufaa yake. Wakfu unaweza kuwekwa kwa mali zifuatazo:-

- a) Mali isiyohamishika kama vile jengo, ardhi, shamba, pesa au nyumba kwa makubaliano ya wanachuoni wote.
- b) Mali inayohamishika kama vile vitabu, nguo, wanyama na silaha; kutokana na athari iliyothibiti kuwa Khalid (R.A) aliweka Wakfu nguo zake za vita na silaha zake zitumike katika kupigania njia ya Mwenyezi Mungu. (Imepokewa na Ahmad, Bukhari, Muslim, Tirmidhiy, Nasai na AbuDaud). Aidha wanachuoni wanakubaliana kuweka Wakfu vitu vya kutandikia Msikitini na taa za msikitini vitu ambavyo sio vya kudumu.
- c) Aidha inajuzu kuweka Wakfu mapambo kwa kuva na kujipamba kwa sababu ni kitu ambacho watu wanaweza kunufaika nacho duniani sawa na wanavyoweza kunufaika na jengo.
- d) Mali zisizoshikika (*intangible properties*) kama vile milki za ubunifu au haki za utaalamu.

2.7.1 Sharti za Kinachowekwa Wakfu

Ili Wakfu uweze kutekelezwa kisheria, kitu kinachowekwa Wakfu ni lazima kitimize masharti yafuatayo:-

- a) Kiwe ni mali yenye thamani.
- b) Kiwe kinajulikana kwa ukamilifu wake, mipaka yake na kadhalika.
- c) Kiwe kinamiliikiwa kikamilifu na Muweka Wakfu wakati wa kuwekwa Wakfu.
- d) Kisiwe katika mali kubwa isiyogawika.
- e) Kisifungamane na haki ya mtu mwengine
- f) Kiweze kutoa manufaa kisheria na kwa mujibu wa urfu (desturi).
- g) Uwekaji wa Wakfu usiwe na masharti, usiwe wenye kutenguka bali uwe wa kudumu na uanze baada ya kutamkwa.
- h) Lengo la uwekaji wa Wakfu liwe linakubalika kisheria kwa kupatikana faida au maslahi maalum.

2.7.2 Umiliki wa Mali iliyowekwa Wakfu

Makusudio ya umiliki hapa ni haki ya uamuzi katika kitu kilichowekwa Wakfu. Zipo kauli mbili za wanavyuoni kuhusiana na nani anakuwa na haki ya uamuzi. Kauli hizo ni kama ifuatavyo:-

- i. Kwa mujibu wa Imam Abu Hanifa uamuzi wa kitu kitabakia kwa muweka Wakfu na manufaa yake yatakwenda kwenye jambo la kheri lililowekewa. Kwa maana hiyo umiliki kamili unabakia kwa muweka Wakfu.
- ii. Ama Imam Malik, Imamu Shafii, Swahibani (Abu Yussuf na Muhamed bin Hassan) wamebainisha kuwa umiliki wa kitu unakuwa ni wa Mwenyezi Mungu na manufaa yake ndio yanatumika katika mambo ya kheri hivyo Muweka Wakfu hatakuwa na uamuzi tena kwa mali aliyoiweka Wakfu.

2.7.3 Kubadilisha Mali ya Wakfu (*Tabdil*)

Kubadilisha au kuuza sehemu au mali yote ya Wakfu ikiwemo ardhi na mapato yanayopatikana kununua mali au ardhi nyengine na kuiweka kuendeleza malengo ya Wakfu wa mwanzo kwa masharti na malengo yale yale. Kubadilisha Wakfu kunakubalika na wanavyuoni walio wengi na madhehebu ya Shafii, Maliki na Hambali iwapo mashati yake na malengo yake yatativizwa.

Kwa msingi huo mali yoyote ya Wakfu ikiwemo ardhi inapokuwa haina tija kiuchumi njia ya kubadilisha inaweza kutumika. Hivyo inaweza kuuzwa na thamani yake ikanunuliwa ardhi nyengine itakayokuwa na manufaa zaidi. Ubadilishaji unaweza kuwa kwa kubadilisha ardhi kwa ardhi, mali au fedha kwa njia inayokubalika kisheria.

Kwa mujibu wa kanuni zilizopo Zanzibar mtu ye yote anayetaka kubadilisha Wakfu ni lazima kwanza aandike barua ya maombi kwa Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana akibainisha sababu za msingi zilizopeleke ombi hilo. Katibu Mtendaji atalihakiki, kulipima na kufuatilia sababu zilizotajwa. Iwapo ataridhika, Wakfu husika kubadilishwa ataomba kibali cha kubadilisha Wakfu huo kutoka kwa Waziri anayesimamia sheria ya Wakfu. Baada ya kupokea kibali cha Waziri ataiomba Mahkama Kuu ya Zanzibar ifute waraka wa Wakfu husika na waraka unapofutwa Kamisheni italazimika kusimamia ubadilishaji wa Wakfu huo na kupatikana Wakfu mwengine pamoja na uandishi wa nyaraka husika.

2.8 Masharti ya Ujumla katika Wakfu

Yapo mambo ya ujumla ya kisheria yanayohusiana na shughuli za Wakfu. Kati ya hayo ni kama yafuatayo:-

- i. Ni lazima Wakfu ufungike na makusudio ya kisheria kwa kuwa ni ibada ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu.
- ii. Kipaumbele katika kunufaika na mali ya Wakfu kiwe ni kwa maslaha ya wale waliowekewa Wakfu.
- iii. Ni lazima mali za Wakfu ziwe ni zenyе kuleta manufaa, ziendelezwe ili ziweze kuhifadhika na kukuza mapato yake na iwapo kutakuwa na ziada ya mapato basi inufaishe kitu kinachokaribiana au kushabihiana zaidi na wanufaika.
- iv. Wakfu unaendana na zama, hivyo unaweza kuhusisha mambo mengi zaidi yanayojiri na yatakayokuja kwa kuwashirikisha maulamaa wa zama husika.

- v. Katika suala zima la kuziendeleza mali za Wakfu kinachotakiwa kuangaliwa ni lenye maslahi zaidi. Katika mfano wa hili Sayyidna Omar R.A alibadilisha matumizi ya Msikiti. Aidha Imam Ahmad R.A aliruhusu kuuondosha msikiti na kuupeleka Mji mwengine kwa vile manufaa ya Msikiti ni kwa Waislamu wote.

2.9 Sura za Wakfu

Wakfu unaweza kuwekwa katika sura nyingi na kila moja inaweza kuwa na baadhi ya hukmu zinazoitofautisha na sura nyengine. Sura hizo na mambo muhimu yanayohusiana nazo ni kama ifuatavyo:-

2.9.2 Wakfu Unaotokana na Wasia

Wakfu wa namna hii una sifa zifuatazo:-

- Unaanza kutekelezwa baada ya mtu aliyeuweka kufariki.
- Unatakiwa usizidi thuluthi moja ya wasia baada ya kutolewa madeni.
- Unaweza kuwa katika mali yoyote.
- Unafungamana na masharti mengine ya mirathi.
- Unaweza kipingwa (*can be challenged*).
- Hauna kinga dhidi ya madai (*claims*).

2.9.2 Wakfu wa Mali Isiyohamishika (*Waqt of Remainder Estate*)

Wakfu huu una sifa zifuatazo:-

- Unaanza mara tu Wakfu unapowekwa.
- Ni wenyewe kudumu milele.
- Una kinga dhidi ya madai.
- Hauna kiwango maalumu cha kuweka kisheria.
- Hauwezi kipingwa.
- Unapaswa kunufaika na msamaha wa kodi.

2.9.7 Wakfu wa Fedha Taslim (*Cash –Waqf*)

Ni aina ya Wakfu ambapo mtu huweka fedha zake ili zifanyiwe mradi ambao utawanufaisha wanufaika au unanufaisha katika kutoa mikopo mema na miradi mingine ya maendeleo. Wakfu huu una sifa zifuatazo:-

- Unabadili umiliki (*transfer of ownership*).
- Una kinga ya madai.
- Hauna kiwango maalumu kisheria.
- Hauwezi kipingwa.
- Unaweza kunufaika na msamaha wa kodi.

2.9.8 Wakfu wa Mapato ya Mali (*Income Property*).

Huu ni Wakfu ambao unatokana na mapato ya kitu ambacho ni haki ya mtu mfano mapato ya haki za ubunifu. Wakfu huu una sifa zifuatazo:-

- Hauna muda maalumu.
- Unatoa manufaa kwa warathi (heirs) au kwa mujibu wa wasia.
- Una kinga dhidi ya madai.
- Hauna kiwango maalumu kisheria.
- Hauwezi kupingwa.
- Una msamaha wa kodi.

2.9.9 Wakfu wa Utumizi wa Majengo (*Real Estate Waqf*)

- Unakusanya misikiti, majengo ya Kiislamu na ya kijamii.
- Unahamisha umiliki.
- Una kinga dhidi ya madai.
- Hauna kiwango maalumu kisheria.
- Hauwezi kupingwa.
- Unanufaika na kodi.

2.9.10 Wakfu wa Familia

- Unakusanya kuhudumia familia na watu wengineo.
- Unahamisha umiliki.
- Una kingi dhidi ya madai
- Hauna mipaka ya kizazi (*generation*) cha kunufaika kisheria.
- Unaweza kupingwa.

2.10 Uhusiano na Tofauti Kati ya Wakfu na Wasia (*Will*)

Uhusiano na tofauti zilizopo katika dhana mbili hizi ni:-

- i. Wakfu ni kuizuwia asili ya mali na kusabilia (kutoa sadaka)manufaa yake; Ama wasia ni kumilikisha kitu baada ya mauti sawa kama ni mali au manufaa .
- ii. Wakfuunalazimisha kudumu wala haijuzu kughairi yaani kubadili uamuzi (kwa kauli ya wanachuoni walio wengi); ama wasia unalazimisha lakini inajuzu kwa aliyeusia kurejea kauli yake kwa mali yote au baadhi.
- iii. Wakfu haupelekei dhati ya kitu kumilikiwa na mnufaika bali unakhasisi kutoa manufaa tu kwa yule aliyewekewa Wakfu ama wasia unahaulisha umiliki na manufaa.
- iv. Kumiliki manufaa ya Wakfu kunadhihirika wakati wowote utakaotajwa na Wakifu sawa kama yuko hai au baada ya kufa kwake; ama umiliki na kunufaika na wasia kunakuwa baada ya kifo cha Muusiaji tu.


2.11 Mahusiano na Tofauti Kati ya Wakfu na Amana (*Trust*)

Uhusiano uliopo katika dhana mbili hizi ni kama ifuatavyo:-

- Katika hali zote mali husika zinahifadhiwa kwa msimamizi.
- Manufaa yake hupewa watu maalumu au hutumika kwa maslahi ya Umma.
- Kazi ya Mdhaminu au Msimamizi ni kuisimamia mali kwa muongozo wa kisheria ili kuleta tija kwa maslahi ya wanufaika na sio kwa maslahi yao binafsi.

Ama tofauti ni kama zifuatazo:-

- Katika sheria za kisekula Mdhaminu wa Amana anahesabika kuwa ni mmiliki wa mali kinyume na msimamizi wa Wakfu yeye hahesabiwi kuwa ni mmiliki.
- Wakfu unakusudiwa shughuli za kheri wakati Amana hailazimishi kuwa katika mambo ya kheri.
- Wakfu unahesabika kuwa ni jambo la kidini, la kheri na la wema wakati Amana hailazimishi hayo.
- Wakfu unalazimisha kuwa wa kudumu ama Amana inaweza kurejeshwa kwa wenywewe.



SURA YA TATU

MAHITAJI YA MABADILIKO KATIKA WAKFU

3.1 Utangulizi

Usimamizi, uendelezaji na matumizi ya mali za Wakfu kwa kipindi kirefu sasa umekuwa hauridhishi na kupelekea kutokupatikana tija iliyokusudiwa. Wakati kuna baadhi ya nchi ambazo utaratibu wa Wakfu umekuwa ukitoa mchango mkubwa katika kutatua matatizo mengi yakiwemo ya upatikanaji wa mitaji, ufadhilli wa masomo, kuchangia huduma za elimu, afya, ustawi wa jamii na hata kujenga miji mipya bado kwa upande wa Zanzibar hali iko duni sana. Hii imesababisa na mambo mengi yakiwemo kukosekana kwa dira na juhudzi za makusudi za kuendesha na kusimamia shughuli za Wakfu kwa mujibu wa hali na mahitaji ya wakati tulionao.

Ili kuleta hali bora na kuufanya utaratibu wa Wakfu kuchangia kwa kiasi kikubwa katika sekta mbali mbali za kiimani, kijamii na kiuchumi ni lazima juhudzi kubwa ichukuliwe ili kubadilisha fikra, mawazo na uelewa wa watu. Aidha katika kujenga msingi madhubuti miradi ya Wakfu itahitaji ufadhilli mkubwa na mchango wa wataalamu wa fani mbali mbali sawa kama ni wa kujitolea au walioajiriwa. Dhana ya Wakfu inahitajika iwe pana zaidi itakayokusanya hata kuweka Wakfu muda na utaalamu wa mtu.

Mabadiliko yanahitajika na ni lazima yafanyike kwa taufiki ya Mwenyezi Mungu. Hakuna wa kuleta mabadiliko hayo ila ni mimi, wewe na kila mwenye imani na uchu wa kuiletea maendeleo jamii yetu. Wale wanaochukua juhudzi katika mambo yao ndio Mwenyezi Mungu huwaongoza katika kuyafanikisha kwa namna iliyo bora.

3.2 Wajibu wa Taasisi Zinazosimamia Wakfu

Msimamizi anatarajiwa kufanya kila kinachopasa ili kuendeleza ustawi wa mali za Wakfu anazozisimamia. Sheria ya Kiislamu inatilia mkazo kuhusu wajibu wake wa kuitunza, kuisimamia na kuitumia mali ili ihifadhi, idumu na kutoa mapato makubwa zaidi ili aweze kutekeleza malengo yake.

Ili kuleta mabadiliko katika Usimamizi wa Wakfu ni lazima taasisi zinazosimamia Wakfu kwanza zilitambue na zibadilike kwa kuzingatia mahitaji, fursa na changamoto zilizopo. Kulinda, kuhifadhi na kuendeleza mali za Wakfu ni wajibu kwa kila Muislamu. Hata hivyo, Taasisi, Asasi

na Jumuiya mbali mbali zenyenye jukumu la kusimamia mali za Wakfu zitalazimika kutekeleza yafuatayo:-

- Kutoa huduma bora katika usimamizi wa Wakfu, kuziendeleza mali zake na kukuza mapato yake.
- Kujenga imani ya wananchi na kushajiisha ili wachangie maeneo mbali ya Wakfu.
- Kujenga uelewa kwa kutafuta maeneo mapya na hali mpya za Wakfu zinazoendena na mahitaji ya zama.
- Kulinda mali za Wakfu na kurejesha zilizopotea.

3.3 Sababu Zinazoathiri Uendelezaji wa Wakfu

Moja ya sababu kubwa zinazoathiri usimamizi na uendelezaji wa Wakfu ni taaluma isiyotosheleza. Wengi wa waweka Wakfu, wasimamizi, wanufaika na hata watumizi wa mali za Wakfu kwa kiasi kikubwa wamekosa taaluma ya msingi katika sheria ya Wakfu na mabadiliko ya shughuli za Wakfu yanayotokana na mabadiliko ya zama na mazingira. Sababu nyenginezo ni kama ifuatavyo:-

- Kukosekana ubunifu na uwajibikaji kwa wasimamizi. Wengi wameridhika na hali iliyopo na kinachopatikana, hivyo hawatafuti mbinu bora za kuendeleza yaliyopo wala kufuatilia tafiti na mambo mapya yanayojiri katika taaluma, usimamizi na uendeshaji wa Wakfu.
- Uchache wa elimu na utambuzi kuhusiana na mambo yanayohusiana na Wakfu.
- Kupotea kwa kumbukumbu na milki za Wakfu nyingi kutokana na sababu nyingi zikiwemo uendeshaji usioridhisha, kutokujua, ubadhirifu na ufisadi.
- Kutokushirikishwa ipasavyo Waislamu (wadau) katika kukagua/kuchunguza namna taasisi za Wakfu zinavyoendeshwa na kutoa njia bora na zenyenye ufanisi za kuendeleza na kuhamasisha uendeshaji na usimamizi wa Wakfu. Hii imepelekea kukosekana uungwaji mkono na mipango endelevu ya kuimarisha nyakfu.
- Athari za usoshalisti zilizoweka kila kitu katika mikono ya serikali na kuwaweka mbali wanachuoni, wanajamii, wawekezaji na watu au taasisi zenyenye lengo la kuimarisha shughuli zinazochangia maslahi ya umma zikiwemo za Wakfu bila ya kujali mipaka ya kijigrafia .
- Mazingira yasiyorafiki kwa uwekezaji katika mali za Wakfu.
- Tabia ya kuwa tegemezi na kutokujiamini katika kubadilika, ikiwemo kubainisha kuwa mali za Wakfu zinaeendeshwa kisoko na sio kwa maslahi mengine.

3.4 Vipaumbele Katika Uendelezaji Wakfu

Si rahisi kushughulikia mambo yote kwa wakati mmoja ili kujenga hali bora ya Wakfu. Ni lazima kuwa na mkakati na kutoa vipaumbele katika ushughulikiaji huo. Inapaswa utoaji wa vipaumbele uwe kwa kukuza mapato ya Wakfu kwa miradi mikubwa yenye malengo ya kutoa misaada ya ujumla kwa jamii. Aidha yanapaswa kuzingatiwa makundi makubwa ya watu hawa

yaliyowachwa kwa muda mrefu kwa mfano Wakfu zenyе lengo la kunufaisha walimu wa madrasa, masikini, kukuza elimu, kuimarisha ustawi wa jamii na mfano wake.

Kabla ya kufanya miradi mikubwa ya Wakfu ni lazima kwanza ufanyike upembuzi yakinifu ili kubaini miradi ambayo inaweza kutoa tija zaidi. Kwa msingi huo haitakikani kubahatisha au kukisia tu bali ni lazima watumike wataalamu halisi kwa mfano wahandisi *wajenzi* (*civil engineers*) ili kuandaa michoro ya majengo, watathmini majengo (*quantity surveyors*) ili kutoa makadirio ya gharama na namna kama hiyo. Taarifa zinazokusanya zitumike kukadiria matarajio ya mapato ya kitega uchumi kwa mwaka. Taarifa hizi zitawezesha kuandaa orodha za mali za Wakfu zinazoweza kuwekezwa na kutoa vipaumbele kwa vile vyenye mapato makubwa.

Uendelezaji mzuri wa mali za Wakfu unaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa juhudzi za kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Aidha unaweza kurejesha juhudzi za kutoa mitaji isiyo na riba katika shughuli mbali mbali za kimaendeleo. Kwa mujibu wa Mahmoud A. Mahdi (2002) wa *Islamic Development Bank*, maendeleo ya mali za Wakfu katika nchi za Ghuba katika kipindi cha 1992-1996 yalizidisha mapato yao kwa 69%, yalizidisha rasilimali zake (*net fixed asset*) kwa 120% na yakaongeza mitaji kwa 79%.

Mpango mzuri wa kuendeleza mali za Wakfu unaweza kupelekea mapato ya mamilioni ya pesa kwa kila mwaka. Kwa msingi huo haitakuwa vyema kuwacha tu kila mtu kuweka vipaumbele vyake. Kamisheni ya Wakfu baada ya kila kipindi ni lazima itoe muongozo mfano kunyanya kiwango cha elimu kuwa ndio kipaumbele. Katika uwekaji wa muongozo huo ni lazima ushirikishe watu wenye taaluma mbali mbali zikiwemo shariah, uchumi, elimu jamii (*sociology*) na wengineo.

Vipaumbele katika Uendelezaji wa mali za Wakfu ni lazima ufanyike na kutiliwa nguvu na Kamisheni. Hatahivyo kuna tatizo linaloweza kujitokeza la kuzidiwa na shughuli katika majukumu yake ya msingi na hivyo kupelekea mengine kutopewa umuhimu unaostahiki. Iwapo hili litatokea patahitajika kuwa na mipango kabambe ya kuwashirikisha watu na Taasisi za nje na waatumish wa kujitolea. Uwekaji wa vipaumbele uzingatie pia kuwepo tatizo la bajeti finyu, ushirikiano mdogo na urasimu wa kiutendaji kwa taasisi zinazosimamiwa na Serikali.

3.4. 1 Mambo ya Kutekelezwa kwa Haraka

Mambo yafuatayo yanataka yashughulikiwe kwa haraka sana katika suala zima la uimarishaji wa shughuli za Wakfu. Mambo hayo ni:

- Kuendeleza ukaguzi na utafutaji wa mali za Wakfu zilizopotea.
- Kuanzisha *database* ya kielektroniki ya mali za Wakfu
- Kuhifadhi maelezo na vielelezo vya Wakfu kwa njia tofauti za kileo.
- Kukuza mapato ya mali za Wakfu na kuziwekeza kwa masharti ya Muweka Wakfu.
- Kupitia vyanzo vya mapato ya mali ya Wakfu.
- Kuhakikisha utekelezwaji wa nyasia za Wakfu

- Kuendesha semina, darsa, warsha na makongamano kuhusiana na Wakfu.
- Kufanya upembuzi yakinifu kwa mali za Wakfu ambazo hazina tija kubwa.
- Kuidhinisha makampuni yaliyohasisi usimamizi na kuendesha Wakfu.
- Kutafuta mali za Wakfu zilizochukuliwa na watu au kwa maslahi ya umma ili zilipwe fidia na kuhaulishwa.

3.4.2 Mipango ya Baadae ya Utekelezaji

Kutokupanga ni sawa na kupanga kuwa pasiwe na mafanikio. Ili tuweze kurejesha nafasi ya Wakfu, upo umuhimu mkubwa wa kutilia mkazo wa Wakfu wa mambo ya kheri. Wakfu wa mambo ya kheri ni istilahi pana ambayo haiishii katika mambo yenye uhusiano wa moja kwa moja na dini bali tuchukue utaratibu wa makusudio ya sheria katika suala zima la Wakfu ambalo linajumuisha ustawi mzima wa jamii. Mambo ya kuzingatia ni:-

- Mitaji na miradi (*Funds & Projects*).
- Kuwa na mfumo mmoja (*Standard forms*).
- Kuwa na chombo madhubuti cha Uratibu.

3.5 Taasisi Zinazotoa Misaada ya Kitaalamu na Mitaji ya Wakfu

Zipo taasisi na asasi nyingi zinazotoa mikopo na misaada ya kitaalamu kwa Wakfu katika ngazi za kitaifa na kimataifa. Ni vyema misaada hiyo na mitaji ikatafutwa na kutumika vyema katika uendelezaji wa Wakfu. Kati ya Taasisi hizo za kimataifa ni:-

- Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (*IDB*)-Jedah-Saudi Arabia.
- Wizara ya Mambo ya Kiislamu Wakfu, Daawa na Miongozo – Saudi Arabia.
- *Kuwait Awqaf Public Foundation*.
- *Kuwait Finance House* – Kuwait.
- Wizara ya Wakfu na Mambo ya Kiislamu- Oman.
- *General Endowment Authority* -UAE.
- Mamlaka ya Wakfu ya Uturuki.

Uendelezaji wa Wakfu usijifunge katika kuchukua mitaji, misaada na ushauri katika nchi na taasisi za Kiislamu tu bali unaweza ukunufaika na kila msaada ambao unakubalika katika sheria ya Kiislamu na ambao hauna nia mbaya. Aidha unweza kuangalia fursa zilizopo nchini na katika kanda hii.

3.6 Mambo Muhimu ya Kuzingatia Katika Kuomba Miradi

Sio kila mradi wenyе nia njema unapata ufadhili au msaada. Ili mradi wa Wakfu uweze kunufaika ni lazima ufikie vigezo. Baadhi ya mambo hayo muhimu ni:-

- i. Upembuzi yakinifu wa kina wa mradi unaokusudiwa utakaobainisha pamoja na mambo mengine:-

- a. Maelezo timilifu ya mradi na yote yanayohusiana nao vikiwemo vipengele vyake, sehemu yake, taratibu za mipango yake na wasfu.
 - b. Gharama za ardhi na ujenzi.
 - c. Ratiba ya utekelezaji wa mradi.
 - d. Utafiti wa mahitaji ya soko kwa mradi.
 - e. Gharama zitakazotumika na faida inayotarajiwa.
 - f. Gharama za Usimamizi na uendeshaji.
 - g. Utafiti wa kifedha na matarajio.
- ii. Maelezo muhimu kuhusiana na Wakfu zikiwemo nyaraka na kopi ya wasia.
 - iii. Maelezo ya msingi kuhusiana na wahuksika wa Wakfu.
 - iv. Ahadi kuwa mradi huo haujatekelezwa na mtu huyo huyo.

3.7 Miongozo Inayohusiana na Kodi

Wawekaji wa Wakfu wanakusudia kusaidia jamii. Kwa msingi huo ni vyema kukawa na utaratibu maalumu wa kutoa misamaha ya kodi kwa miradi ya Wakfu na wawekezaji wakubwa katika miradi mikubwa ya Wakfu ambayo inalenga kunufaisha watu wengi. Hivyo suala la kodi linaweza kuangaliwa katika njia mbili:-

- i. Taasisi za Wakfu kupata msamaha wa kodi kwa vile lengo lake kuu ni kuisaidia jamii.
- ii. Mtoaji (*donor*) kupata baadhi ya misamaha kwa kutoa kwake katika taasisi za Wakfu kwa vile sehemu ya mapato yake yanainufaisha jamii.

3.8 Nyenzo za Mafanikio katika Shughuli za Wakfu

Nyenzo muhimu za mafanikio ni sababu zote zinazoiwezesha tasiya ya Wakfu kufanikiwa katika kutekeleza dira na dhamira yake ya kuurejeshea nguvu utarabibu wa Wakfu. Kwa vile kumekuwa na taarifa nyingi za kutokufaulu, kutokuendesha vyema na ujisadi hivyo ni muhimu kuweka hatua za maendeleo. Ni lazima Serikali ishirikiane na taasisi mbali mbali za kijamii ili kuhakikisha kuwa juhudhi za kufufua Wakfu zinapata nguvu kubwa ya pamoja. Hatua zinazo hitajika ni kama zifuatazo:-

3.8.1 Dira na Uongozi

Ni lazima kuwa na viongozi waadilifu, wachapa kazi wenye dira na uwezo wa kuipeleka ahazi inakokusudia kwenda. Kiongozi ni lazima awe tayari kujitolea ili aweze kumudu na kuhimili tufani na mikondo katika safari yake. Cha muhimu zaidi kiongozi anapaswa awakumbushe mara kwa mara wasaidizi wake na mabaharia wake kuhusiana na lengo lao ili wasije kusahau na kupotea njia.

3.8.2 Uhamasishaji wa Wadau na ushirikishwaji:

Wadau wa tasiya za Wakfu ni lazima waainishwe. Kimsingi Waislamu kwa ujumla wao, wanufaika na wasimamizi wa mali za Wakfu ndio wadau wakubwa ambao taasisi ya Wakfu

itahitaji kuungwa mkono nao. Adha wadau wengine wanaopaswa kuzingatiwa ni viongozi wa kiislamu katika ngazi mbali mbali, Taasisi za kijamii, Serikali, jumuiya za wataalamu na za wafanyabiashara, wanataluma, wanahabari, wanasiasi na taasisi za elimu. Mdau mwengine muhimu sana ambae anatakiwa kushirikishwa tokea hatua za awali ili ajuwe dira iliyopo ni taasisi za kifedha za Kiislamu zikiwemo benki za Kiislamu, Mashirika na wakala wa Bima za Kiislamu , mashirika na mifuko ya Kiislamu. Kuungwa mkono na kundi hili kutasaidia sana katika kupanga, kuongoza na kukuza uwekezaji. Wadau ni lazima wakumbatiwe ili waweze kuleta mchango mkubwa katika maeneo yao.

3.8.3 Umilikishwaji wa Jamii

Kuifanya jamii kuamini kuwa ni wahusika wa Wakfu ni muhimu sana katika kulinda na kuendeleza mali za Wakfu. Ni sawa na biashara ambayo wahusika wote hutaka ipate faida wakiamini kuwa kufanikiwa kwa biashara hiyo ndio kufanikiwa kwao. Katika kufanikisha hili ni lazima kuteuliwe baadhi ya viongozi wa kijamii wenyewe ushawishi mkubwa ili wawe wadhamini wa shughuliza Wakfu katika maeneo yao.

3.8.4 Sera na Sheria Zinazotoa Nguvu kwa Shughuki za Wakfu:

Ni lazima kuwepo Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo madhubuti katika shughuli za Wakfu. Sheria zitoe nafasi kwa mabadiliko mapya yakiwemo kuruhusika kuchangia katika Wakfu kupita mishahara, uhifadhi wa mali za Wakfu na kutoa msamaha wa kodi kwa mali za Wakfu au kusamehewa baadhi ya kodi kwa wachangiaji wakubwa wa mifuko ya Wakfu.

3.8.5 Mitaji:

Ni lazima kuwepo na mitaji katika hatua za kuanza na kundeleza shughuli za Wakfu. Kazi ya maboresho ya shughuli za Wakfu ni lazima isaidiwe katika kugharamia shughuli za kiutendaji na kujenga uwezo. Kasi ya mabadiliko kwa kiasi kikubwa itategemea uwezo iliokuwa nao Kamisheni katika kazi zake mbali mbali zikiwemo huduma kwa wateja, miradi, miundo mbinu ya kiutendaji, mishahara na maposho ya watendaji, na mazingira ya kazi.

3.8.6 Uwekezaji:

Kadiri taasisi za Wakfu zitakavyokuwa na nguvu na zikaongeza mali na nitaji yake hapo ndio sera bora za uwekezaji ndio zinaweza kufanya. Kufanya vibaya katikauwekezaji, au kupata hasara kunadumaza shughuli za Wakfu kwa ujumla wake.Aidha kabla ya uwekezaji ni lazimakufanyike upembuzi yakinifu.

3.8.7 Viongozi, watendaji na Wafanyakazi:

Viongozi, watendaji na wafanyakazi wote lazima wawe na stadi, elimu, uwezo na uwajibikaji wa kutekeleza dira, dhamira na malengo ya taasisi.

3.8.8 Ubia

Ubia ni muhimu sana katika kupelekeea (i) uhaulishaji wa ujuzi na stadi. (ii) Kuunganisha baina ya taasisi zeny shughuli na malengo yanayofanana na (iii) kukusanya stadi na nyenzo pamoja ili kujenga nguvu itakayopelekea mafanikio zaidi.

3.8.9 Msaada wa Kitaalamu

Kupata msaada endelevu wa kitalamu ni muhimu sana kwa kuhakikisha ufanisi wa taasisi ya Wakfu hasa katika maeneo yenye upungufu wa taaluma au bajeti ndogo. Mfano wataalamu wa teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuhakikisha kuwa mifumo inapatikana na iko katika hali njema.

3.8.10 Tabia na Maadili ya Kazi

kwa kuzingatia kuwa taasisi za Wakfu zinatokana na mfumo wa Kiislamu hivyo zinahitajia kuwa na daraja kubwa ya maadili na tabia njema ambazo ni lazima ziongoze taasisi na wafungamane nazo watu wake. Washirika wa maendeleo na jamii kwa ujumla wanataka kupata uhakika kuwa michango, fedha na misaada yao iko salama na haihujumiwi kwa ubadirifu, rushwa na ujisadi.

3.8.11 Kuleta Mabadiliko

Inahitajika misaada inayotolewa iwe ni yenye kuwawezesa wananchi kiuchumi. Mpe mtu jembe na ataweza kula maisha yake. Hivyo miradi yote ya Wakfu ilenge kuwafanya watu kuwa wazalishaji, wabunifu, wanaojitegemea na sio wategemezi.

3.8.12 Masoko:

Masoko ndio yanayopelekeea kufanikisha kuleta tija na maendeleo. Tunaweza kuwa na bidhaa bora kabisa lakini kama haziuziki ni lazma tutafeli. Mafanikio halisi ya miradi ya Wakfu yanapimwa kwa namna tutakavyofanikiwa kuhamasisha watu kutoa mitaji kwa ajili ya Wafu na na watu watakavyohamasika kuweka Wakfu. Baadhi ya mikakati ya kuleta masoko ni kama ifuatavyo:-

(i) Bidhaa za Wakfu Bidhaa za Wakfu zinaweza kufungwa na kutangazwa kwa wanunu. Mfano wa bidhaa hizo ni 1% ya mshahara au pato la mwezi; Kiwango maalumu cha mali (*Lump Sum*); Wakfu w Mali; Wakfu wa Biashara; Wakfu wa Wasia. Kila moja katika njia hizi ina utaratibu wake wa kuweka Wakfu. Ni lazima kuwe na ubunifu mpya katika njia za kuweka Wakfu.

(ii) Kuendeleza aina za Wakfu: Pamoja na Wakfu wa familia na jamii kuna pia Wakfu za taasisi na vyama. Pana umuhimu mkubwa wa kuzingatiwa namna Taasisi za kiraia zikiwemo zinavyotaka kukaa nafasi ya Wakfu. Taasisi za Wakfu zinaweza kuwa pia katika mfumo wa Bodi.

(iii) Kulenga Masoko (watu): Ni lazima kuwe na wataalamu na utaalamu katika kutafuta na kupanga mikakati ya mafanikio. Ni lazima watu washajiishwe ili wapende kuweka Wakfu na watumie vyema kwa ukweli na uadilifu mali za Wakfu.

(iv) Kampeni, Elimu na Uhamasishaji: Mikakati ya aina mbalimbali inaweza kutumika katika kuhakikisha mafanikio ya kukuza mikakati ya masoko: Mazungumzo katika Redio; vipindi vya televisheni; makala katika majarida na magazeti; Khutba za Ijumaa na darsa za misikitini; Semina na mikutano; mitaala ya skuli na madrasa; wahasibu, wanasheria na wachumi, mitandao ya wanaojitolea kozi maalumu za vyuo, benki za Kiislam na mazungumzo na makundi mengineyo. Kwa kuzingatia hali ya ulimwengu panahitajika kuwepo kwa tovuti itakayowezesha mchango wa mtandaoni kufanya tafiti kwa maeneo maalum, kuchapisha tafiti, kuweka maeneo ya majaribio; kutafuta fursa za masoko katika mazingira ya nje kwa kuwa wa kwanza kuanzisha mambo yenye manufaa makubwa; ushirikishaji wa makundi makubwa ya watu; kutoa huduma maalumu za ushauri wa mambo ya Wakfu; Kutumia fursa za matukio maalumu; kujitangaza, kujenga uhusiano na ushirikiano mzuri nje na ndani ya nchi; kujenga uhusiano bora na jamia na wenza wote.

3.8.13 Kufungamana na Taratibu za Kishariah (*Shari'ah Compliance*):

Kwa vile Wakfu ni mfumo wa Kiislamu ni lazima upate msaada na nguvu ya washauri wa shariah ya Kiislamu. Zaidi ya hapo wakaguzi wa Kishariah watahitajika ili kuhakikisha taratibu za kishariah zinatekelezwa katika uwekezaji na matumizi sahihi ya mitaji. Kufungamana na taratibu za kishariah kunahesabika kuwa ni msingi mkubwa na kichocheo muhimu cha mafanikio.

3.8.14 Utawala Bora:

Katika zama hizi ambazo ubadhirusi na rushwa vimeongezeka katika utawala wa mambo ya kifedha suala la utawala bora linapokosekana huleta hasara na mvurugiko mkubwa. Mashirika makubwa yamefilisika kwa sababu ya ubadhirusi na rushwa, hivyo taasisi za Wakfu ni lazima zitanabahi ili zisije kushindwa. Mifano bora (*best practice*) iliyopo ya utawala katika fedha na uwekezaji ni lazima ifuatwe bila ya kusita. Uwazi bila ya kutoa siri (*transparency*), uwajibikaji, kukagua na kupima (*checks and balances*), kuwazungusha watendaji na wafanyakazi na udhibiti wa ndani (*internal control*) na mfano wa hayo ni lazima yazingatiwe.

3.9 Mambo Muhimu Katika Kuleta Mabadiliko

Wakfu ndio msingi mkuu wa misaada ya kheri katia Uislamu. Suala linalojitokeza ni kwa nini jamii ya Kiislamu inapaswa kulichukulia suala la kuleta mabadiliko katika utekelezaji wa Wakfu kuwa ni la lazima na lipewe kipaumbele katika utoaji wao wa misaada? Ni mambo yepi yatakayo washajiisha makundi mbalimbali ya watu wakiwemo wafanyakazi, wataalamu, wanawake, wanafunzi, vijana, wafanyakazi, wakulima, wafugaji, wavuvi na wengineo kuweka Wakfu? Kuleta mabadiliko katika Wakfu kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kijamii na uvezeshaji wa

wanajamii kunahitajia nyenzo na motisha. Nyenzo na motisha hizo zinaweza kuwa ni tofauti na zile zinazotumika katika kuhimiza nguzo ya fardhi ya Zakka. Utafiti zaidi utahitajika kufanywa katika eneo hili la vipi watu wataweka Wakfu za kheri kwa hiari. Hata hivyo, mambo mengi yanaweza kupatikana kuwa ni nyenzo za msingi na motisha muhimu katika masoko yanayokusudiwa na yanayozingatiwa katika kutoa zawadi kwa khari kwa Mwenyezi Mungu. Baadhi ya mambo ya kuzingatiwa ni kama yafuatayo:-

3.9.1 Uchambuzi wa Hali Halisi (*Situation Analysis*):

Uchambuzi wa hali halisi ni nyenzo inayotuwezesha kufahamu kwa upana kuhusiana na jamii fulani. Mchakato pia utatuwezesha kupanga mikakati ili kukidhi mahitaji yaliyopo. Uchambuzi huu unapaswa kufanywa kitaalamu kwa kuwashirikisha kikamilifu watu wa jamii husika. Aidha uchambuzi ni lazima uambatane na kujua nguvu, udhaifu, fursa na vitisho vilivyopo.

3.9.2 Kushughulikia Mahitaji ya Jamii

Ili tuweze kuleta mabadiliko yenye tija katika utaratibu wa Wakfu ni lazima kuainisha na kushughulikia mahitaji makubwa yaliyomo katika jamii. Tukiangalia kwa kina katika historia tutakuta kuwa Wakfu zilikuwa zinawekwa ili kushibisha mahitaji ya jamii sawa kama yalikuwa ni ya kibinadamu, kimazingira, kielimu, tafiti, mahitaji ya mazishi, kuwasaidia waee wasiojiweza, watu wenye ulemavu na wanaoishi katika mazingira magumu. Mahitaji ya jamii yanaweza kupatikana kupitia uchambuzi wa hali halisi.

3.9.3 Matumizi ya Quran na Hadithi:

Wakati wa zama za mwanzo za Uislamu Kitabu na Sunna vilikuwa ni vichocheo muhimu katika nidhamu ya Wakfu. Imepokewa kuwa mara baada ya kuteremshwaaya zinazohimiza kutoa masahaba wengi walianza kutoa mali zao zilizo bora kabisa, aidha utoaji huu ulilenga kuwasaidia jamaa wa karibu, mayatima, wahitaji, wanaoomba na kwa ajili ya kuendeleza dini. Aidha kuna mifano mingi iliyothibiti katika sunna kuhusiana na utoaji.

3.9.4 Historia ya Kiislamu:

Imepokewa kutoka kwa Saad bin Zuraarah amesema: Simjui Sahaba yelete wa Mtume wa Mwenyezi Mungu katika walioshiriki vita vya Badri miiongoni mwa Muhajirina na Ansari ambae hakuweka kitu kuwa Wakfu. Waliviwekea masharti kuwa visiuzwe, visirithiwe, na wala visitolewe zawadi mpaka sikuya kiama. (Ahkaamul Awqaaf uk.8-9). Aidha imeripotiwa na Jabir kuwa masahaba wote ambao walikuwa na uwezo wa kiuchumi walijiwekea Wakfu. (*Ibn Qudàma.n.d. al-Mughnî. vol. 9-598.*)

3.9.5 Kutaja Mifano Bora ya Kuigwa

Kuna mifano mingi ya watu walioweka Wakfu za aina tofauti hapa kwetu na nje ya nchi ambayo inapaswa kuigwa. Mfano wa hapa kwetu ni Wakfu wa Qureishi kwa ajili ya hospitali ya wagonjwa wa akili, wakfu wa Fedheluu Salim kwa ajili ya shughuli za kielimu na kijamii nk.

Ama kwa upande wa nje ya nchi tunaweza kuangalia nyakfu zifuatazo:-



Nyumba ya makazi na maduka, iliyoko wilaya ya Al Khan, Sharjah, UAE. Aliyeweka Wakfu ni Mtawala wa Sharjah, Msimamizi ni Mamlaka ya Wakfu ya Sharjah na wanufaika ni masikini wa visiwa vya Comoro.



Ghorofa 13 zenyе maofisi zilizoko Chittagong, Bangladesh, ambazo zimefadhilliwa na APIF Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IDB) kama ni mkopo wa muda mrefu.



Makazi ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Moulay Ismail, Meknes, Morocco, kimefadhliliwa na APIF (IDB) kwa mkopo wa miaka 30.



Shamba la Mifugo la Wakfu – Iran

3.9.6 Kuvutia Wafadhili: Miradi ya Wakfu inayofaulu katika zama zetu hizi ni ile inayowavutia wafadhili. Hata hivyo ipo miradi inayoanzishwa lakini ikakosa kuungwa mkono na wafadhili lakini ikawa inafufua moyo wa Wakfu na kuleta faida kubwa japo baada ya muda. Cha msingi ni kufanywa utafiti wa kina na kujenga hoja. Kwa mfano kuanzisha Wakfu wa chuo cha amali kwa ajili ya vijana walio katika mazingira magumu.

3.9.7 Miradi ya Kiibada: Ni vyema miradi ya ujenzi wa nyumba za kiibada kama vile misikiti na madrasa mpya au miradi ya kijamii kama skuli zisiachwe katika mipango ya Wakfu. Hii ni kwa sababu miradi hii ina nafasi kubwa ya kuzishajiisha nyoyo za wanajamii waweze kuchangia katika miradi mikubwa ya Wakfu.

3.9.8 Ukarimu na Nia Njema: Ukarimu ni sifa ya msingi kwa Waislamu. Ukarimu huongezewa na nia njema ya kusaidiana, kujali wengine, na kupendana. Haya ndio yanayopelekea wengine kuchangia kwa ajli ya wenye kupatwa na majanga, wengine kwa kutarajia radhi za Allah tu,

wengine ni kushindana katika kutenda mema, wengine kuwaondoshea watu mahitaji na mfano wa hayo.

3.9.9 Wakfu ni Mtaji: Kinyume na mambo mengine ya kheri ambayo huwa yanatumika moja kwa moja Wakfu siku zote unatumika na kubakia kuwa kama ni mtaji sawa kama ni fedha taslim au rasilimali. Kwa msingi huo manufaa ya Wakfu huwa yanabakia daima mpaka mtaji umalizike au uwe hauna thamani tena.

3.9.10 Kuonekana na Kuweka Kumbukumbu Nzuri: Kazi inayofanywa na taasisi ya Wakfu ni lazima ionekane na wale waliota mali zao kuziweka Wakfu. Kwa lugha nyengine watoaji na wafadhili hupenda waone kinachofanyika kwa mali na rasilimali zao. Haya yataonekana iwapo kutaimarika majengo au zitakuwa bora zaidi hali za wanufaika. Taarifa za mara kwa mara ziwe zinatolewa kwa wafadhili ambapo ndipo watatoa zaidi. Siku zote mafanikio ndio yanayoleta mafanikio zaidi.

3.10 Nafasi ya Wakfu Katika Kupunguza Umasikini

Umasikini kwa maana pana tunaweza kusema ni ile hali ya mtu kutokuishi maisha ya kiheshima kama mwanadamu. Hali hii inasababishwa na kukosa rasilimali au/na uwezo wa kupata mahitaji yake ya msingi. Umasikini ni kikwazo cha kufikia maendeleo ya kimwili, kiakili na kimaadili, kiasi cha Mtume S.A.W kuushabihisha na ukafiri.

Uislamu unashajiisha wafuasi wake kuupiga vita umasikini kwa njia mbali mbali zikiwemo kutoa zaka, sadaka, kuzalisha mali na kufanya kazi kwa lengo la kujitegemea. Kwa msingi huo tutaona Uislamu unapiga vita umasikini kwa kuhimiza kujituma na kufanya kazi kwa juhudhi. Aidha unatoa mitaji na rasilimali kwa kuhimiza walionacho kutoa kwa njia ya Zakka na Sadaka. Wakfu ni sehemu ya sadaka kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu *"Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi (kwa kusali tu peke yake) Bali wema hasa ni (wa wale) wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Malaika na Kitabu na Manabii na wakawa wanawapa mali juu ya kwamba wanayapenda jamaa na mayatima na Masikini (walioharibikiwa) na waombao na katika kuwakomboa Watumwa na wakawa wanasmamisha Sala na kutoa zaka na watekelezao ahadi zao wanapoahidi, na wavumiliao katika shida na dhara na katika wakati wa vita; hao ndio waliosadikisha (Uislamu wao) na hao ndio wanaomcha Mungu.* (Baqarah:177)

Uislamu una lengo la kumkomboa mwanadamu. Ukombozi huo unakuja katika itikadi na mambo yote ya maisha yanayogusa jamii, uchumi na siasa. Mambo haya yanakwenda sambamba na yanategemeana katika kumjenga mwanadamu. Mamlaka ya Wakfu inapaswa kutoa nguvu na msukumo ili:-

- Taasisi za Kiislamu ziweze kutekeleza wajibu na mipango yake kwa mujibu ya mahitaji ya wakati tulionao.

- Ziwe na watendaji wenyе uwezo wa kubuni na kutenda kwa ufanisi.
- Kuwa na nyenzo na teknolojia inayohitajika katika zama zilizopo.
- Kuwa mazingira bora ya kiutendaji.
- Kujenga ajira.
- Kuendeleza viwango vya hali za maisha.
- Utoaji wa huduma njema za Afya.
- Uzalishaji bora wa huduma za kielimu, chakula na nyumba.

Hivyo Wakfu unaweza kuwekwa katika maeneo yote ambayo inakubalika kупelevka sadaka zikiwemo katika shughuli za kidini, kijamii, kielimu, kiafya, kimalezi, kiuchumi na kimazingira. Katika nchi za Kiislamu kuna skuli nyingi, madrasa, vyuo na taasisi za elimu ya juu, hospitali, vituo vya mayatima, watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wazee wasiojiweza, misikiti na hata mifuko ya udhamini wa masomo ambazo zinaendeshwa kwa mali ya Wakfu.

3.11 Nafasi ya Wakfu katika kukuza Ujasiriamali

Uwezeshaji kwa njia ya kutoa mitaji mdogo mdogo (*micro-finance*) ni nguzo madhubuti ya kupambana na umasikini pamoja nakuleta maendeleo ya jamii. Lengo kuu la uwezeshaji huu ni kutoa mitaji inayoweza kubebeka kwa watu wenyе kipato kidogo. Hali hii kwa mtazamo wa wachumi wengi inaonekana kama ni kujitia hatarini; hivyo shughuli hii imedharauliwa na vyombo vingi vya kifedha na mabenki ambavyo vimemili katika kutoza riba.

Kuna mambo manne ambayo mara nyingi ndio yanayopelekea kuongezeka kwa riba katika baadhi ya mikataba ya ukopeshaji inayotolewa na taasisi za fedha. Mambo hayo ni:-

- i. Gharama za mitaji.
- ii. Gharama za uendeshaji.
- iii. Uwezekano wa hasara katika kukopesha ukilinganisha na faida inayotakiwa kwa ajili ya kutunisha mfuko.
- iv. Matarajio ya kukua kwa mtaji.

Kutokana na sababu hizi ndio mara nyingi gharama za taasisi zinazotoa mikopo zinakuwa kubwa. Kukosekana miundombinu ya ulipaji kumezifanya taasisi hizo kushughulikia zaidi muamala wa fedha taslim na mzunguko wa fedha halisi.

Nidhamu ya Wakfu inaweza kutumika kufidia uendelezaji wa Ujasiriamali. Taasisi zinazotoa mitaji midogo midogo (*Islamic Microfinance*) zinaweza kutumia fedha za Wakfu au Zaka kwa ajili ya kuzieneza kwa wale wenyе mahitajio makubwa kutokana na umasikini wao. Katika hali hii kutahitajika uhamasishaji wa uwekaji Wakfu utakaotumika kwa shughuli za kukopesha. Lengo kubwa la kuangalia kwa hapa ni ile faida inayopatikana kwa kuwawezesha watu kuongeza vipato vyao kwa kuwapatia mitaji. Watu watakaonufaika na mikopo hii watahamasishwa kuchangia katika Wakfu husika ili watu wengi zaidi wanufaika hasa

unapozingatia kuwa thamani ya pesa mara nyingi hupungua. Njia maarufu inayotumika kwa sasa katika kufanikisha hili ni Wakfu wa pesa taslim.

Kwa vile muundo huu utatamalaki na mgawanyo wa kitakachopatikana, hivyo mara nyingi huwa na faida kwa pande mbili, endelevu na unaweza kupunguza kutokulipwa kwa mikopo iliyotolewa na utumiaji mzuri wa mitaji itokanayo na Wakfu. Mifumo ambayo inaweza kutumika katika kuwakopesha wajasiriamalini kama hivi ifuatavyo:-

- i. Njia ya *Qard al Hasanah* yaani mkopo wa kusaidiana ambao hauna gharama zozote.
- ii. Njia ya mtazamo wa kibiashara unaoendana na faida kama vile:-
 - ✓ Njia ya Murabaha, Ni njia ya kununua bidhaa baada ya kuagizwa na mteja na baadae bidhaa hiyo huuziwa mteja na Mnunuzi baada ya kutia faida ndogo kwa mujibu wa soko na bidhaa iliyonunuliwa.
 - ✓ Njia ya *Bai'mua'jal-* njia ambayo manunuzi yanafanywa na malipo yanafanywa baadae.
 - ✓ Njia ya *Salaam*, Hii ni njia ya mkataba wa ununuzi wa bidhaa ambapo fedha hulipwa mwanzo na bidhaa hiyo hupatikana kwa kipindi na muda fulani (baadae). Njia hii mara nyingi hutumika kwa ununuzi wa mazao.
- ✓ Njia ya Mudaraba/*Musharaka*, Njia hii ni ya kushirikiana katika biashara ambapo mmoja hutoa fedha na mwengine hutoa ujuzi au mkutekeleza muamala wenyewe.

3.12 Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Katika Wakfu


Matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika uhifadhi na usimamizi wa mali za Wakfu ni jambo la lazima kwa zama tulizonazo. Database ya Usimamizi wa mali za Wakfu inapaswa kuwa na maelezo yote muhimu ya Wakfu yakiwerwemo yafuatayo:-

- Mfumo wa maelezo ya usimamizi wa Wakfu (*Waqf Information Management System*).
- Mfumo wa ujenzi bora wa taarifa (*Comprehensive Building Information system*)
- Mfumo wa taarifa kwa kuzingatia Joigrafia (*Information System based on Geographic information System*).
- Mfumo wa Jiografia ya visiwa vya Unguja na Pemba(*Zanzibar Geographical Information System*).

3.13 Utaratibu wa Wakfu Zisizohamishika

Katika uwekaji wa Wakfu zisizohamishika, muweka Wakfu atalazimika kuusajili Wakfu wake katika Mamlaka ya Wakfu (Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana) akiwashuhudisha mashahidi wanaokubalika kisheria. Kupitia Mamlaka ya Wakfu ndio kutafanyika mawasiliano yanayohusiana na mali za Wakfu kwa taasisi nyenginezo za nje. Muweka Wakfu anaweza kuteua msimamizi wa Wakfu atakayetambuliwa na kusajiliwa na Mamlaka ya Waku. Aidha Mamlaka ambayo ndio mdhamini mkuu wa Wakfu inaweza pia kuwa ni msimamizi. Wajibu wa

Msimamizi utakuwa ni kuizalisha mali ya Wakfu na kuiendeleza pamoja na kuwapatia wanufaika haki zao wanazostahiki kwa mujibu wa wasia.



3.14 Wakfu wa Muda Maalumu

Wapo baadhi ya Watu wanaopendelea kutoa Wakfu kwa muda maalumu. Sura za Wakfu huu ni kama ifuatavyo:-

- Mtu kumiliki kitu na kukiweka Wakfu kwa muda maalumu. Mfano aseme :-
 - ✓ Nyumba yangu nimewawekea Wakfu wanafunzi kwa muda wa miaka mitano.
 - ✓ Gari yangu ni Wakfu wa wagonjwa kwa siku za mapumziko.
- Mtu mwenye ujuzi mfano daktari bingwa kuweka muda au siku maalumu:-
 - ✓ Akaukhasi kwa kundi maalumu la watu bila ya malipo.
 - ✓ Akasema kuwa malipo yanakusanya yanufaishe kundi maalumu.

Kwa wanaotaka kutoa muda au vitu kwa muda ni lazima apatikane muweka Wakfu; msimamizi, kitu kilichowekwa Wakfu, makubaliano (Ikrari), wasia unaobainisha makusudio ya kilichowekwa Wakfu na muda wa Wakfu.

3.15 Wakfu Wa Fedha Taslim (*Cash Waqf*)

Kama tulivyoona inawezekana Wakfu ukawekwa kwa kitu ambacho sio cha kudumu kama vile mti, mnyama, gari na kadhalika. Baada ya utafiti imeonekana pia kuwa watu wanaweza kuweka pesa taslim kuwa ni Wakfu.

Wakfu wa fedha taslim unakuwa kwa kukusanya kiwango cha fedha kutoka wa waanzilishi na kutengeneza jambo linalokubalika kisheria ambalo litawanufaisha wanufaika kwa njia ya kudumu. Aina nyengine ya kunufaika kwa Wakfu huu ni kutumika pesa zenyewe kwa kuwapatia mikopo wajasiriamali, wanafunzi, watu wenye mahitaji maalumu ya dharura na kadhalika. Katika njia ya pili wapo baadhi ya wanachuoni wanaotilia shaka uhalali wake kwa sababu uwezekano wa kuziendesha aina hizi za mali za Wakfu zikaweza kudumu bila ya kuziwekeza katika mifumo inayotumia taratibu za riba unakuwa ni mgumu.

Mfano mzuri ni kuwa mnamo mwaka 1905 Baraza la Privy la India liliweka sheria ya kutokuruhusu Wakfu wa pesa. Hata hivyo sheria hiyo haikuchukua muda kwani sheria mpya ya mwaka 1913 iliruhusu Wakfu wa pesa. Hukumu hii ya pili ilitumika pia Bangladesh, Pakistan Myanmar na nchi nyingi za Kiislamu. Pamoja na hayo, bado zipo nchi za Mashariki ya kati ambazo hazikubaliani na aina hii kwa hoja kuwa uwekezaji wake hausalimiki na mfumo wa riba. Katika nchi za Misri, Iraq, Syria, Iran, Uturuki, Singapore na Indonesia wameegemea fatwa ya Imam Zufar iliyotolewa karne ya 18 kuwa rasilimali ya Wakfu wa pesa inapasa kuwekezwa katika njia ya *murabaha* na mapato yake ndio yatatumika kwa mujibu wa malengo ya muwekezaji.

Ni vyema zikaanzishwa hati maalumu za Wakfu kuitia mabenki ili kukusanya Wakfu wa Pesa. Miongoni mwa malengo ya Wakfu wa pesa ni:-

- Kuziwezesha Benki na taasisi za fedha za Kiislamu kuwa karibu zaidi na waumini na kuziunganisha na taasisi za Wakfu.
- Kusaidia kukusanya misaada (shahada zinawezwa kutengenezwa hata kwa majina ya watu, familia au jumuia)
- Kubadili ukusanyaji na uchangiaji wa shughuli za kijamii.
- Kusaidia kukuza mitaji ya shughuli za kijamii.
- Kukuza uwekezaji wa kijamii.
- Kushajiisha uhamasishaji wa wenye uwezo kuelewa majukumu yao kijamii kwa kuendeleza shughuli za kijamii katika sehemu zao.
- Kuunganisha usalama wa kijamii na ustawi wa jamii.
- Vivutio vya kupata wateja katika Taasisi za fedha za Kiislamu.


Kuna namna nyingi ambazo zinaweza kutumika katika kukusanya fedha kutoka katika jamii za Waislamu kwa Wakfu wa fedha zikiwemo:-

- Kutumia misikiti (na msikiti unaweza kuwa mwangalizi wa Wakfu zao).
- Maofisa Mauzo
- Mishahara inayopitia Taasisi za fedha za Kiislamu
- Madirisha ya Benki (zilizosajiliwa rasmi).
- Kampuni za Bima ya Kiislamu na Mifuko ya Makampuni yanayoendana na Shariah ya Kiislamu.
- Masokoni, Madukani, Posta na Taasisi zinazotoa huduma za kibashara.
- Taasisi binafsi na za Serikali (Waajiriwa).


Katika kufanikisha hili Muweka Wakfu anaweza kuchangia Wakfu kwa kuweka pesa taslim kwa kuitia taasisi za kifedha zilizoteuliwa na Mamlaka ya Wakfu. Muweka Wakfu ataandika barua kuwa anataka kuchangia Wakfu kwa njia ya fedha taslimu na msimamizi kuitia taasisi za kifedha atatoa shahada ili kuonesha fungu alilochangia, madhumuni na wanufaika katika Wakfu

huo. Taasisi za kifedha zitatoa taarifa hizo kwa Mamlaka ya Wakfu. Aidha Msimamizi atakuwa anatoa taarifa za Wakfu anaousimamia kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa na Mamlaka ya Wakfu.

Utaratibu wa kusajili na kutoa ripoti za Wakfu zisizohamishika ikiwemo Wakfu wa fedha taslim utakuwa kama ifuatavyo:-



Utaratibu wa Wakfu wa Fedha Taslim unakuwa kama ifuatavyo:-




Msimamizi wa Wakfu ataanzisha mradi wa Wakfu na kuwamasisha watu kuwa na hisa katika mradi huo ambaa utakuwa unawanufaisha watu maalum. Mfano linajengwa jengo kubwa la Wakfu litakalokusanya kumbi za mikutano, maduka na dakhalia. Gharama za nyumba hiyo zikakadiriwa kuwa shillingi bilioni moja na wanufaika wakawekwa kuwa ni mayatima, wazee wasiojiweza na wagonjwa. Hivyo msimamizi atakusanya michango ya watu na kila mmoja atapewa shahada inayobainisha fungu lake katika Wakfu huo kwa kuzingatia asilimia aliyochangia katika mradi mzima. Aidha makundi ya wanufaika yatapata gawio la manufaa yao kwa kuzingatia asilimia ya mchango uliotolewa kwa ajili yao.


Mbali na manufaa tuliyoyataja faida inayopatikana katika Wakfu wa pesa inaweza kutumika kusaidia familia masikini, kuendeleza shughuli za kielimu na kiutamaduni mfano kugawa vitabu, kufadhili tafiti maalumu , kuendeleza programu za elimu, nafasi za masomo, misaada kwa maskuli, kuhifadhi na kuendeleza maadili. Aidha zinaweza kuendeleza mambo ya afya na

mazingira kwa watu masikini, kusaidia vituo vya Afya, kutoa madawa na matibabu ya rahisi. Pia zinaweza kutumika kwa kutoa huduma za kijamii, kama majengo, vituo kwa ajili ya shughuli za kidini, kusawazisha maharibiko ya kitabia na mmong'onyoko wa maadili.

Benki za Kiislamu, Bima za Kiislamu (takaful) na mifuko ya Kiislamu inaweza kuwa waendeshaji na wasimamizi wa mtaji wa Wakfu baada ya waweka Wakfu kuisajili katika Mamlaka ya Wakfu kwa utaratibu ufuatao:-



Mamlaka ya Wakfu inaweza kuwa ni mfadhili wa Taasisi za Fedha za Kiislamu ili ziweze kutekeleza malengo ya Wakfu kwa utaratibu ufuatao:-



3.16 Uwekaji wa Wakfu Kupitia Makampuni ya Bima ya Kiislamu (Takaaful)

Kampuni za Takaful zinaweza kuanzisha utaratibu maalumu wa kuweka Wakfu kupitia wateja wake. Chini ya utaratibu huu, watu wa daraja zote wanaweza kushiriki na kuweka Wakfu. Na kwa upande mwengine utaratibu huu huwavutia wengi kuweka bima.

Mpango wa Wakfu kupitia Bima ya Kiislamu ni mpango unaowawezesha watu kukusanya fedha ambazo baadae hutumika katika utaratibu wa Wakfu. Katika mpango huu mchangiaji atakuwa na kiwango maalumu cha pesa ilizokusanywa katika takaful ambazo kiutaratibu hulipwa kila baada ya muda fulani. Fedha hizi ambazo ni haki ya mchangiaji zinakuwa zinatumika katika Wakfu mara zinapofikia muda wake wa kugawiwa.

Mara nyingi wakala wa Takaful huamua kiwango cha fedha za kuchangia na muda wa kuwiva bima yake. Aidha ataamua namna ya uchangiaji mfano kupitia mshahara, kupitia amri ya benki (*bank standing instruction*) au kulipa moja kwa moja. Pia ataeleza taasisi ya kunufaika na Wakfu wake kwa mfano mfuko wa misikiti, elimu, mayatima na kadhalika.

Muamala huu unafanyika kwa mkataba maalumu na makubaliano (*akdi*) ya kufuatwa na namna ya kugawana faida. Akdi zinazotumika ni:

- *Murabaha Mutlaq*: Ambapo shirika la Bima (Takaful) na mtoa mtaji hukubaliana kuwa fedha zitumike katika biashara au uwekezaji bila ya kuweka mipaka.
- *Tabaaruu*: ambapo mshiriki huchangia kiwango kidogo cha pesa kwa ajili ya kujenga mshikamano, udugu, au ushirikiano na wenzake.

3.17 Wakfu wa Miliki za Ubunifu (Intellectual Properties)

Hadi miaka ya karibuni mali zilizojulikana kisheria ziliwuwa ni mali zeny kushikika tu (*tangible properties*). Mizunguko ya kibiashara ilizingatia aina hizo za mali kama ni zeny kumuwezesha mkopaji wa benki na muweka dhamana mbali mbali kuweka dhamana kwa mali hizo. Ama mali zisizoshikika (*Intangible properties*) zilichukuliwa kama dhana nyengine isiyo na nafasi katika hesabu za mali. Kutokana na kukua kwa mizunguko ya kibiashara na kukua sayansi na teknolojia imegundulika kwamba mali zeny thamani kubwa katika ulimwengu wa sasa wa biashara ni mali za ubunifu ambazo ni mali zisizoshikika.

Mali za Ubunifu pamoja na yote yanayoambatana nazo mfano alama za biashara (*trademarks*), haki za uvumbuzi wa kisayansi, ubunifu wa maumbo (*industrial designs*), hakimiliki (*copyrights*), viashiria vya maeneo na haki zinazotokana na mikataba yake zinaweza kutumika katika kuweka dhamana, Wakfu, kutoa hidaya na mfano wa hayo. Mali hizo zinamilikiwa na mvumbuzi wake au aliyehamishiwa na mbunifu. Kimsingi jina la mali za ubunifu ndilo ambalo linatengeza uhusiano wa kihisia (*emotional link*) katika matumizi ya mali husika na ndio lenye thamani ya kuiwezesha mali husika kuwa na thamani ya kuwekwa Wakfu. Ili mali hizi ziwekwe Wakfu ni lazima zisajiliwe kwanza, hati ya usajili ndio inayopaswa kuwekwa dhamana ya Wakfu.

3.18 Usimamia wa Ardhi za Wakfu

Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika kulikuwa na ardhi nyingi na mashamba yaliyowekwa Wakfu katika miji ya Unguja na Pemba. Kutokana na sababu mbali mbali na katika zama mbali mengi ya mashamba hayo yamepotea. Hata hivyo mbele ya Allah na uso wa sheria mashamba hayo yatabaki kuwa ni wakfu madhali taratibu rasmi za kuyahaulisha hazikuchukuliwa.

Zanzibar imeshuhudia maendeleo katika nyanja nyingi lakini maendeleo haya yanapaswa pia kuzigusa na nyanja za dini ikiwemo Wakfu. Kwa upande wa ardhi za Wakfu zilizopo, kuna njia ambazo zinaweza kusaidia kuziendeleza kama ifuatavyo:-

3.18.1 Njia za Kisheria

Mamlaka ya kimahkama (*jurisdiction*) kuhusiana na Wakfu zimo katika Mahkama ya Kadhi na Mahkama nyenginezo za Zanzibar. Hata hivyo kuna kesi za Wakfu ambazo hufika na kuhukumiwa na Mahkama ya Rufaa ya Tanzania. Kwa msingi huu kuna haja ya sheria ya Wakfu kuweka wazi ili iwe rahisi kwa Mamlaka husika kuweza kutoa haki kwa kuzingatia sheria –

Mfano maana ya Wakfu, masharti yake, aina zake, uwekaji, usajili sahihi na Mamlaka ya Kamisheni ya Wakfu. Mambo yote haya yawepo katika Sheria, Kanuni na Miongozo. Kamisheni kupitia kwa Waziri husika pia itayarische na ichapishe katika Gazeti rasmi mali zote na vtega uchumi vya Wakfu zikiwemo ardhi ambazo zitatawaliwa na sheria ya Wakfu.

3.18.2 Njia za Kiutendaji:

Miongoni mwa majukumu ya Kamisheni ni kuhakikisha kuwepo usimamizi yakinifu na wenyetija wa mali za Wakfu. Kamisheni ina wajibu wa kupanga, kuratibu na kuchunguza mambo yote yanayohusiana na Mali za Wakfu. Ni wajibu wa Kamisheni kutoa muongozo wa uendeshaji na usimamizi wa Ardhi za Wakfu. Lengo la muongozo liwe ni kutoa taratibu zenye viwango maalum vya kisheria, muhtasari wa sheria zinazotawala ardhi za Wakfu na ufanuzi wake, uwazi wa taarifa za Wakfu na kutoa utaalamu katika uendelezaji wa ardhi za Wakfu. Muongozo ubainishe:-

- Faida na manufaa ya Wakfu wa Ardhi, masharti, nguzo na taratibu za kubadilisha ardhi ya Wakfu.
- Taratibu za kusajili ardhi za Wakfu, kuhaulisha au kufuta Wakfu.
- Usimamizi wa ardhi za Wakfu zikiwemo utaratibu wa kulipa, uendeshaji, bima (takaaful) na kubadilisha.

Ardhi za Wakfu zinapaswa kusajiliwa ili ziweza kuangaliwa, kuhamiwa na kuhifadhiwa vyema. Aidha ubunifu wa kuzitumia ardhi hizo ili zilete tija zaidi unahitajika. Yapo mashamba mengi yanayotumika kwa kilimo, ufgaji na kadhalika lakini Wakfu husika umekuwa haupati manufaa yoyote. Hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kubuni njia bora za kuzitumikia ardhi hizo kibashara ili kuleta tija.

Kwa kuzingatia malengo ya Wakfu shughuli nyingi zinaweza kufanyika zikiwemo ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, maduka, maghala, vituo vya Afya, vituo vya elimu, uchapaji na mfano wa hizo. Kupata muwafaka na ushauri kutoka Mamlaka zinazohusiana na shughuli zinazotaka kufanyika ni lazima kupewe aulawia. Pamoja na maendeleo yanayoweza kupatikana haiwezi kukatalika kuwa kuna vikwazo na changamoto ambazo zitajitokeza katika uendeshaji, utekelezaji na usimamizi.

Ili kuwa na udhibiti mzuri na kumbukumbu muhimu ni lazima ardhi zote za Wakfu sawa kama ni za Misikiti, vituo vya elimu, makaburi, shughuli za kheri au maeneo ya wazi zisajiliwe na nakla za kumbukumbu zake zipatikane Kamisheni ya Wakfu. Kwa ardhi ambazo zimegeuka miji au zimetoka katika usimamizi au matumizi ya Wakfu kwa njia zisizo za kisheria ni lazima zifidiwe kwa taratibu zilizopo ili kuzihaulisha kisheria. Tutambue kuwa bila kuhaulishwa, mbele ya Mwenyezi Mungu bado ardhi hizo zitahesabiwa kuwa ni Wakfu na wanaozitumia wanabeba dhima na jukumu kubwa kisharia.

3.18.3 Njia za Matumizi

Ardhi za Wakfu ni lazima zibainishwe kwa uwazi matumizi yake, wanufaika na malengo yake. Pia zibainishwe mali zilizomo na hali yake, kama nazo zinafuata Wakfu husika au vyenginevyo. Ili kuleta tija Wakfu unaweza kubadilishwa matumizi kwa mfano shamba la miembe kukodishwa kwa kiwanda cha sukari ili kupandwa miwa na wanufaika wa Wakfu kupata fungu maalumu kutoka katika kiwanda.

Uendelezaji wa matumizi ya ardhi za Wakfu unaweza kuingia katika hali mbili kuu:-

i) Njia isiyo ya kisheria ambayo inaweza kuwa katika:-

- Kuipatia mitaji miradi ya Wakfu: Ni vyema zikatumika njia za Kiislamu katika kuipatia mitaji miradi ya Wakfu. Njia hizo zinaweza kuwa ni Murabaha, Ijarah, Ijara wal-Iqtinaa, Salam, Istithna na mikataba mingineyo. Aidha zinaweza kutumika njia za Mudharaba, musharaka nk.
- Kubadilishana utaalamu baina ya Taasisi za Wakfu
Kutokana na fursa za utandawazi inapendekezwa taasisi za Wakfu za ulimwenguni zishirikiane. Ushirikiano wa taasisi hizo utapelekea ubadilishanaji wa utendaji bora, usimamizi mzuri, michakato endelevu, misaada ya kitaalamu, na kubadilishana uzoefu. Taasisi hizo zinaweza kuwa wizara, idara, taasisi za kielimu na mashirika ya kikanda na kimataifa. Pia kumekuwa na fursa ya uratibu wa shughuli za kuendeleza na kuwekeza Wakfu wananchi za nje kwa kushirikiana na wenza wengine.
- Kufufua ardhi za Wakfu zisizo na tija kwa kuzibadili .

ii. Njia za kisheria:

Kupitia na kuweka wazi maeneo ya sheria za Wakfu ili kuondoa migongano ya kisheria na kuipa nguvu sheria ya Wakfu iweze kutawala mali zote za Wakfu.

3:19 Usimamizi wa Nyumba za Wakfu

Lengo kuu la usimamizi wa Wakfu ni kuleta tija kwa wanufaika pamoja na kuhifadhi mali yenye ya Wakfu ili iweze kudumu. Iwapo mali ya Wakfu itaingia hatarini na kupotea au itabaki lakini haitaleta tija basi ni lazima hatua madhubuti zichukuliwe katika kuihami na kuendeleza. Hili linaweza kufanyika kwa kupitia njia mbili zifuatazo:-

3.19.1 Njia za Kisheria

Mikataba ya ukodishaji wa nyumba ni lazima itolewe katika muda unaotakiwa na ichunge hali ya soko, maslahi ya Wakfu na matumizi ya nyumba kutokwenda kinyume na Sheria za Kiislamu na maadili mema ya jamii yetu. Yote hayo yapewe nguvu za Kisheria kwa kutiwa katika Sheria, Kanuni na Miongozo.

3.19.2 Njia za Kiutendaji

Nyumba za Wakfu ni lazima ziwekewe kumbukumbu zake zote zinazohusiana na:-

- Wakfu: zikiwemo wasia husika, Mweka Wakfu, Msimamizi, Wanufaika, wakati wa kunufaika, namna ya kunufaika na kama hayo.
- Hali ya nyumba: ikiwemo ramani yake, ukubwa wake, matengenezo yanayofanyika na gharama zake, pahala ilipo, matumizi yake, fursa na hatari zinazoikabili nyumba, muda wa kukaguliwa nyumba.
- Mpangaji, watu wanaoitumia nyumba pamoja na mpangaji, muda anaopaswa kulipa kodi, kuchukua mkataba, kukaguliwa, kutekeleza au kutekelezewa jambo lolote la ziada lililomo au ambalo halimo katika mkataba.

3.20 Kuchagua Taasisi Inayofaa Kuipatia Fedha za Miradi ya Kuendeleza Mali ya Wakfu

Mambo ya kuzingatia katika kuchagua taasisi inayofaa zaidi ni kama ifuatavyo:-

- a) Mikopo yenyе riba isizingatiwe kabisa katika kuchagua taasisi ya kutoa mitaji. Ni lazima tuangalie vyema mahitaji mawili yanayopingana:-
 - ii. Mahitaji ya mtoaji fedha anayetaka kupata faida kwa fedha aliyoivekeza.
 - iii. Mahitaji ya msimamizi wa Wakfu aliyezungika kuona kuwa manufaa ya Wakfu na umiliki unabakia katika masharti ya Wakfu na kuridhiwa na Mwenyezi Mungu.

Iwapo hatutamridhisha anayetoa fedha atakataa kuazima fedha kwa kunufaisha Wakfu na iwapo tutashindwa kulinda matakwa ya Wakfu makubaliano yatakayofikiwa yatakuwa ni batili. Hivyo ni lazima tuchague taasisi inayozingatia masharti ya sheria na inayochunga maslahi ya pande mbili.

- b) Njia za kutoa mikopo ya fedha zenye manufaa madogo . Njia hizi ingawa zinaweza kutoa faida kubwa na zinaweza kuwasaidia watu lakini hazitaweza kuwa na maslahi makubwa katika kuendeleza Wakfu. Njia hizo ni :-

i. Mkopo wa Mursad

Huu ni mkataba ambao msimamizi anakubaliana na mkopeshaji kutoa fedha ili kuihuisha au kuifanya matengenezo mali ya Wakfu ambayo haina mtaji. Baada ya makubaliano hayo msimamizi hutoa mkataba wa muda mrefu (*long lease*) utakaomuwezesha mkopeshaji kujilipa au kujifidia gharama alizotoa. Mfano kulipa thuluthi moja na kujifidia thuluthi mbili. Mikataba hii ilikuwa inatumika sana katika karne ya 18 na 19 lakini kwa sasa kidogo kidogo imekuwa inawachwa. Mkataba wa hadi miaka 10 unaweza kukubalika kwa lengo la kuujenga upya Wakfu lakini sio wa muda mrefu sana, kwani mkataba huu hautokuwa na maslaha kwa Wakfu. Aghalabu katika mkataba huu si mpangaji wala msimamizi ambae huchukua uangalizi wa karibu

na hivyo Wakfu kujikuta umetelekezwa. Kwa msingi huu ni vyema kuachana na mkopo huu kwa vile unaonekana kumpendelea zaidi mkopeshwaji kwa gharama za Wakfu.

ii. Hukr

Huu ni mkataba ambao mpangaji hulipa kodi ya muda mrefu kwa kutanguliza ambayo hutumika kwa kuifanyia matengenezo au kuikuza mali ya Wakfu na sehemu ndogo hutekelezewa malengo ya Wakfu. Haki hii inaweza pia kurithiwa na ilitumika sana katika zama za Dola ya Othmania (*Ottoman empire*). Hata hivyo, kutohana na athari zake mbaya kwa mali za Wakfu, aina hii ya mkataba ilizuiliwa katika miaka ya 1950 na 1960 katika nchi za Misri, Syria, Irak, Jordan, Libya na nyenginezo. Kimsingi tunapoangalia kwa kina tutakuta kuwa hakuna uwiano wa kimaslahi kwa pande mbili.

iii. Mudhaaraba (kugawana faida na hasara).

Ni hali ambayo mmoja hutoa mali (*rabul mali*) ya kuwekeza na mwengine huifanyia kazi (*mudhaaribu*) na mwisho wanagawana faida kwa mujibu wa asilimia walizokubaliana. Kimsingi katika mkataba huu hasara anaipata aliyetoa mali ya mtaji kwa sababu mudharibu anachotoa yeye ni ujuzi wake na muda wake. Hata hivyo mudharibu akifanya uzembe basi itamlazimu kulipa alichosababisha kupotea.

Taasisi ya Wakfu haina ujuzi maalumu wala si kazi yake kufanya biashara na wala haiwezi kugawana mapato na muwekezaji kwa mkataba wa muda mrefu hivyo haiwezi kufanya mudhaaraba mwengine na mtu wa tatu. Aidha si rahisi kumpata muwekezaji ambae atakubali kutoa mtaji wa kuendeleza mali ya Wakfu kwa sharti kuwa hasara yoyote atabeba yeye tu. Pamoja na yote hayo lengo kuu la Wakfu ni kupata manufaa ili yatekelezewa wasia wa Wakfu na sio kufanya biashara. Kwa msingi huo mudhaaraba si njia nzuri ya kuendelezea mali za Wakfu.

iv. Sukuk(cheti) au Bondi

Wazo la msingi katika Bondi za Benki za kawaida ni kuwa miradi mikubwa huwa inahitaji kiwango kikubwa cha fedha. Inawezekana fedha hizo kukusanya kutoka kwa watu wengine wa mataifa, daraja na dini mbali mbali. Hufanya kwa watu hao kupewa bondi ambazo ni sawa na cheti cha mkopo. Mtu mwenye bondi hawezikuzifanya lolote fedha zilizokusanya. Kwani fedha alizozitoa ni sawa na mkopo na hupewa faida maalumu sawa kama aliyekusanya fedha amepata faida au hasara. Kwa msingi huu muamala huu umeambatana na riba na hivyo haukulaliki kisheria.

Kwa upande wa sheria ya Kiislamu kuna *sakk* na wingi wake ni *sukuk*. Sukuk inamaanisha umiliki wa kitu kilichopatikana. Iwapo muwekezaji Muislamu atanunua sukuk hupata fursa ya kushiriki katika mradi wa uwekezaji. Mwenye sukuk hupata fungu lake la faida ingawa haina kiwango maalumu wala uhakika wa kupatikana. Sukuk hufanyiwa biashara hivyo biashara yake ni lazima

ifanywe kwa mujibu wa sheria za Kiislamu. Kuendeleza Wakfu kwa kutumia sukuk kutaleta tija pale tu kiwango maalumu cha fedha kilichopangwa kukusanya iwapo kitafikiwa. Ni muhimu kuzingatia kuwa miradi ya sukuk haiingizwi katika miradi yenyewe uwezekano mkubwa wa hasara.

v) Istis-naa (*Commissioned Manufacturing or construction work*)

Huu ni mkataba ambao upande mmoja unanunua bidhaa au kitu (kama jengo) kwa upande mwengine na upande wa pili unalitengeneza kwa sifa maalumu na kwa malipo maalumu yaliyopangwa mwanzo lakini yanalipwa pale bidhaa inayolipwa inapokuwa tayari kutumika. Iwapo benki itaisimamia kazi yenyewe ni sawa na pia inaweza kuingia mkataba. Mkataba huu unaitwa “*parallal Istisna*” au “*Back to back istisnaa*” Katika mkataba huu Wakfu hautopoteza kwa sababu Benki inabeba dhamana ya kiwango cha kazi na sifa walizokubaliana mwanzo.

vi) Musharakah (ushirika)

Ushirika uko wa aina mbili:-

- Ushirika katika umiliki: Ambapo kila mmoja ana sehemu ya umiliki katika mali moja mfano nyumba iliyorithiwa kwa pamoja au kitu walichokipata watu wawili na zaidi kwa pamoja (Aina hii haina mnasaba na mada).
- Ushirika wa mkataba ambapo watu waliokatibiana kukusanya rasilimali zao pamoja kwa kutarajia kupata nguvu zaidi . Aina hii pia imegawika makundi mawili.
 - ✓ Ushirika usio na mipaka (*sharikat al-mufawadha*), unaokusanya kuwa deni la mmoja wa washiriki basi huwa linawahusu wote na muda wa kumalizika ushirika hautajwi (ushirika huu pia hauna *maslahi na hauwezi kutekelezwa katika Wakfu*).
 - ✓ Ushirika wenge mipaka (*sherikat al-inan*) – Ni ushirika ambao watu wanagawana faida na hasara kama walivyokubaliana na deni lolote aliloingia mmoja wao litamruhusu yeye binafsi yake. Ushiriki huu ni mzuri kwa vile unajengeka kwa makubaliano ambayo huchunga masharti ya Wakfu. Hata hivyo kimsingi Msimamizi sio mmiliki hasa wa mali ya Wakfu bali inamilikiwa na Mwenyezi Mungu na kwa msingi huo kuna ugumu wa kutumia njia hii katika kuendeleza mali za Wakfu.

vii). Musharakah Mutanaqisah

Katika aina hii maalumu ya ushirika, taasisi ya Wakfu inayotaka mtaji wa kuendeleza mali ya Wakfu na taasisi inayotoa mtaji wanakubaliana kuanzisha mradi wa pamoja ambapo kila upande unakuwa na sehemu ya fungu. Fungu la taasisi iliyotoa fedha linapungua kila baada ya kipindi kwa kuuza hisa zake kwa Wakfu mpaka mwishowe mradi wote unabaki kuwa ni wa Wakfu. Wakati mradi unapobakia katika Wakfu taasisi ya fedha inakuwa tayari imeshajilipa na pia imepata na faida inayokubalika. Katika mkataba huu ni lazima wahusika wajiepushe na kuweka mikataba miwili ndani ya mmoja. Hivyo kila mkataba uwe peke yake. Utaratibu huu siku zote unapelekea kila upande kupata faida.

SURA YA NNE
UENDESHAJI WA MALI ZA WAKFU NA AMANA
(Kwa Mujibu Wa Sheria Namba 2 Ya 2007- Kifungu cha 16 hadi 31)

4.1 Uwezo wa kusimamia Mali za Wakfu (Kifungu cha 16)

Kamisheni ya Wakfu imepewa Uwezo wa Kusimamia kama mdhamini mali zote za Wakfu ambazo kabla ya kutumika kwa Sheria hii ziliwa ziwe chini ya usimamizi wa Kamisheni ya Wakfu. Pale ambapo mali yoyote ilikuwa iwe chini ya usimamizi wa Kamisheni ya Wakfu, lakini haikuwa kwa sababu yoyote ile ikisimamiwa na Kamisheni bila ya kujali kitu au jambo lolote itakuwa inasimamiwa na Kamisheni.

Kamisheni imetakiwa kuchukua hatua zote za lazima ili kuzirudisha katika utaratibu wa Wakfu mali zote za Wakfu na kuchukua usimamizi wa ujumla kisheria kwa mali hizo. Katika kufanikisha hilo Kamisheni itatoa taarifa ya siku zisizozidi mia moja na thamanini (180) kwa msimamizi/mwandalizi wa mali ya Wakfu ili kuipeleka mali hiyo Kamisheni katika siku na tarehe iliyowekwa.

Mtu yejote atakayekwenda kinyume na amri hiyo au atakayeizua Kamisheni kurejesha mali ya Wakfu atakuwa ni mkosa na ikithibitika hivyo Mahkamani anaweza kupewa adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kishochozidi miaka mitano.

4.2 Kufanya Wakfu Binafsi (Kifungu cha 17)

Wakfu binafsi wowote uliowekwa kabla ya kuanza kutumika kwa sheria Namba 2 ya 2007 utalazimika kusajiliwa upya Kamisheni na muhusika atalazimika kutoa maelezo yote yanayohusiana na Wakfu huo na hali yake.

Kamisheni haitatoa kinga au huduma yoyote ya kisheria kwa Wakfu binafsi mpaka uwe umesajiliwa na Kamisheni. Aidha Wakfu binafsi wowote utakaowekwa baada ya kuanza kutumika kwa sheria hautatambuliwa kisheria kama hautasajiliwa na Kamisheni.

4.3 Utenguzi wa Baadhi ya Wakfu (Kifungu cha 18)

Hakuna Wakfu wowote utakaotekelawa iwapo nia yake inahusisha malipo ya fedha zozote au manufaa au kutekeleza jambo nje ya Zanzibar mpaka Kamisheni itoe ridhaa ya wazi ya utekelezaji wa nia hiyo.

4.4 Usajili wa Wakfu Binafsi (Kifungu cha 19)

Kamisheni italazimika kuweka daftari la usajili wa mali zote za Wakfu zikijumuisha majengo, ardhi na milki kwa utaratibu maalumu utakaofafanuliwa na Kamisheni. Aidha kama kuna mali zozote zilizojegwa au kuwekezwa katika ardhi za Wakfu pia zitasajiliwa. Watu wote wanaomiliki

majengo yaliyoko kwenye ardhi za Wakfu au wakiwa wanatumia ardhi ya Wakfu kwa namna yoyote ile watalazimika kusajili milki na matumizi hayo haraka sana Kamisheni kwa kutoa maelezo yanayohusiana navyo kama itakavyohitajika na Kamisheni.

Hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa kutumia ardhi au mali yoyote iliyowekwa Wakfu bila ya kwanza kupata ridhaa ya maandishi ya Kamisheni. Ikitokezea kwa jengo lolote kutumika bila ya ruhusa hiyo, Kamisheni inaweza kutaka kubomolewa kwa jengo hilo bila ya kulipa fidia. Taarifa ya kuhaulisha umiliki wa jengo lolote katika ardhi ya Wakfu itatolewa kwa maandishi kupelekwa Kamisheni na muhaulishaji ndani ya siku thalathini za uhaulishaji huo, na kumbukumbu zake zitawekwa kwenye daftari la Usajili wa Wakfu.

Mtu yeyote atakayeshindwa kufuata lolote katika masharti ya kifungu hiki atakuwa ni mkosa na ikithibitika Mahkama inaweza kumpa adhabu ya kulipa faini isiyozidi shillingi milioni mbili au kifungo kisichozidi miaka miwili.

4.5 Uwezo wa Kutaka Mahesabu Yanayohusiana na Mali ya Wakfu (Kifungu cha 20)

Kamisheni inaweza kumtaka mdhamini au mtu yeyote anayedhibiti au kushikilia mali yoyote ya Wakfu kutoa maelezo ya udhibiti wake au uendeshaji wa mali hiyo. Kwa niaba hiyo inaweza kumtaka mdhamini au mtu huyo kuwasilisha vitabu vyovypote au nyaraka, ziwe za hesabu au vyenginevyo kuhusiana na mali hiyo, iliyoko kwenye udhibiti au dhamana yake.

4.6 Kuchukua Udhibiti wa Mali ya Wakfu katika Mazingira Maalumu (Kifungu cha 21)

Kamisheni itakuwa na uwezo wa kuchukua udhibiti wa mali yoyote ya Wakfu endapo itathibitika kuwa mdhamini aliyepo anakwenda kinyume na matakwa ya Wakfu au kinyume na sheria. Kabla ya kufikia uamuzi huo Kamisheni itapaswa kutoa fursa ya kujitetea kwa mdhamini huyo. Kamisheni inapochukua udhamini wa Mali inaweza kutoa amri itakayochapishwa katika Gazeti, kuhusiana na kuiweka mali hiyo katika usimamizi au uendeshaji wa Kamisheni au kuteua mdhamini au wadhamini watakaoisimamia mali hiyu kwa niaba yake.

Mtu yeyote ambaye ameathirika na amri hiyo anaweza kukata rufaa kwa Waziri anayehusika kutaka suala hili lizingatiwe upya.

4.7 Uendeshaji wa Mali za Wakfu (Kifungu cha 22)

Mali zote za Wakfu zilizoingia kwa njia yoyote ile katika udhibiti wa Kamisheni zitaendeshwa kwa mujibu wa makusudio ya Muwekaji wa Wakfu huo; madhali matumizi hayo ni halali na yamethibitishwa kwa ushahidi tosha kwa mujibu wa Shariah na sheria.

Kamisheni inapoona kuwa makusudio hayo hayatekelezeki, hayako wazi, ni kinyume na sheria au imetekeleza ipasavyo lakini yapo mapato yaliyobakia inaweza kuweka utaratibu bora zaidi wa kusimamia mali au mapato hayo ya ziada, kwa utaratibu mzuri, kisheria na kwa matumizi ya sadaka kwa faida ya Muwekaji Wakfu kama itakavyoona inafaa.

4.8 Kuuza Mali za Wakfu Katika Hali Maalum (Kifungu cha 23)

Iwapo Kamisheni itathibitishiwa na ikaridhika kuwa nia ya Muwekaji wa Wakfu haiwezi kutekelezeka ipasavyo, itakuwa ni halali kwa Kamisheni baada ya kupata idhini ya Waziri, kuiiza mali ya Wakfu na mapato ya mauzo yatatumika kuweka Wakfu mbadala na kwa utaratibu uliobainishwa katika kifungu cha 22.

4.9 Uchukuaji wa Mali za Wakfu (Kifungu cha 24)

Hakuna mkataba, makubaliano au amri ya aina yoyote inayokusudia kuuza, kukodisha au kuchukua mali yoyote ya Wakfu kwa kipindi chochote kinachozidi mwaka mmoja itakayokuwa sahihi au halali isipokuwa idhini ya maandishi ya Kamisheni iwe imepatikana kabla. Bila ya kujali sheria yoyote iliyopo inayoelezea vyenginevyo, hakuna hati ya umiliki wa mali ya Wakfu itakayotolewa kuanzia tarehe ya sheria hii kwa mtu au watu wowote kwa sababu ya umilikishaji mbaya au agizo.

4.10 Usitishaji wa Muda wa Mikataba ya Ukodishaji (Kifungu cha 25)

Kwa madhumuni ya kuiwezesha Kamisheni kusimamia ipasavyo mali za Wakfu na Amana, mikataba yoyote ya ukodishaji wa mali za Wakfu na amana inasitishwa kuanzia siku mia tatu na sitini za kuanza kutumika kwa sheria hii; iwe ukodishaji umefanywa kihalali au la na iwe ni ukodishaji, ukodishaji ndani ya ukodishaji au leseni. Usitishaji wa ukodishaji huu utakuwa na nguvu iwe kumetolewa taarifa ya usitishaji huo au la.

Kamisheni, ndani ya siku thalathini tokea kuanza kwa sheria hii, itatoa taarifa ya usitishaji kwa wapangaji au wakodishwaji wote wa mali.

4.11 Kuongezwa Mikataba Mipy ya Ukodishaji (Kifungu cha 26)

Kamisheni itatayarisha mikataba mipy ya ukodishaji ambayo itazingatia:-

- (a) Wapangaji waliopo kisheria;
- (b) malipo ya kodi kulingana na bei ya soko iliyopo;

- (c) mapitio ya kila mara ya kodi;
- (d) malipo ya papo hapo na ya awali yanayofaa.

4.12 Muda wa Kukodisha Mali ya Wakfu (Kifungu cha 27)

Hakuna ukodishaji wa mali ya Wakfu na Amana utakaokuwa kwa kipindi kinachozidi mwaka mmoja mpaka idhini maalumu ya Bodi ipatikane na kwa hali yoyote kipindi hicho hakitazidi miaka mitano. Ukodishaji wowote wa mali ya Wakfu au Amana ambao utakuwa kwa zaidi ya miaka mitano utakuwa ni batili kwa kipindi chote.

Malipo ya ukodishwaji wa mali za Wakfu na Amana yanaweza kupitiwa upya na Bodi kwa masharti na namna iliyoelezwa katika mkataba wa ukodishaji. Bila ya kujali sheria yoyote, mapitio ya kodi hayataekewa mipaka isipokuwa kwa utaratibu ulioelezwa ndani ya sheria hii na mkataba wa ukodishaji.

Ukodishaji wa mali za Wakfu na Amana ikiwemo upangishaji uliofanywa ndani yake hautahusika na mipaka iliyowekwa ndani ya sheria ya Bodi ya kudhibiti kodi za nyumba. Bila ya kujali sheria yoyote inayoeleza vyenginevyo, mgogoro wowote ukiwemo wa uvunjaji au usitishaji wa mpangaji wa hukumu ya kuhama kuhusiana na mali ya Wakfu na mali ya Amana, itashughulikiwa na Mahkama ya Mkoa. Mgogoro au kutokubaliana kokote kati ya Kamisheni na mpangaji juu ya mapitio ya kodi utaamuliwa na Waziri anayehusika.

4:13 Utumiaji Mbaya wa Mali ya Wakfu na Amana (Kifungu cha 28)

Itakuwa ni kosa kwa utumiaji wowote mbaya wa mali ya Wakfu au Amana ukiwemo:-

- (a) Kumkodisha mtu mwengine kusikoruhusiwa na au chini ya mkataba wa ukodishaji.
- (b) Ufichaji wowote wa mali ambao unauwezesha upande wowote au mtu mwengine kufanya faida au kupata manufaa yaliyojificha.
- (c) Utumiaji wowote wa mali ulioelezwa ambao unamuwezesha mtu ye yoyote kufanya faida au manufaa yaliyojificha, itakuwa ni kosa.

Ofisa ye yoyote wa Kamisheni au mtu ye yoyote aliyeingia mkataba au anayefanya kazi kama wakala wa Kamisheni iwe ameteuliwa rasmi au laa ambae atafanya kosa lililotajwa katika aya ya juu ya kifungu hiki akipatikana na hatia atapata adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miaka miwili, zaidi ya faini na kifungo hicho ataamriwa kuilipa Kamisheni kima chote cha fedha kilichopatikana.

Mtu ye yoyote, zaidi ya waliotajwa katika aya ya (2) cha kifungu hiki, ambae atatenda kosa chini ya aya ya (1) ya kifungu hiki, akipatikana atapewa adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua mwaka mmoja; zaidi ya faini na kufungo hicho, mtu huyo ataamriwa kuilipa Kamisheni kima chote cha fedha kilichopatikana.

4.14 Uendeshaji wa Wakfu unaofanywa na Mtu Binafsi (kifungu cha 29)

Kamisheni inaweza kuingia katika makubaliano na mtu yeyote, kampuni au shirika kusimamia mali yoyote ya Wakfu kwa mujibu wa masharti ya makubaliano hayo. Makubaliano yoyote yatakayofanywa yataidhinishwa kwanza na Bodi na yatakuwa kwa muda usiozidi miaka kumi pamoja na fursa ya kuengeza muda kwa uamuzi wa Kamisheni.

4.15 Mali ya Amana na Sadaka (Kifungu cha 30)

Kamisheni itashughulikia mali yoyote ya amana kwa mujibu wa nia na mamlaka ya amana. Pia inaweza kuizua kama amana mali yoyote ya sadaka na kuisimamia mali hiyo kwa mujibu wa masharti ya amana. Usimamizi huo utakusanya mali zote za amana za Kiislamu na sadaka hapa Zanzibar au mali yoyote ya aina hii nje ya Zanzibar ambazo masharti yake na manufaa yake yote ni sadaka kwa Zanzibar.

Katika kutekeleza kazi zake chini ya kijifungu hiki Kamisheni itakuwa na uwezo wa:-

- (a) Kuingilia kati na kuchukua udhibiti wa muda wa mali pale itakaporidhika kwamba mali haisimamiwi ipasavyo, inatumiwa vibaya, kuna mgogoro katika usimamizi wake kiasi ambacho inahatarisha mali au imekuwa ikisimamiwa kinyume na masharti na madhumuni ya amana;
- (b) Kusajili mali zote na kutoa hati ya usajili ikiwa katika muundo kama utakaoelezwa na kanuni zilizowekwa na Bodi;
- (c) Kutoa maelekezo, taarifa na miongozo ya uendeshaji wa mali hizo kadri Bodi itakavyoona inafaa;
- (d) Kufanya jambo jengine lolote linaloambatana na au ni lazima kwa uendeshaji mzuri wa mali hizo.

4.16 Misiki na Madrasa (Kifungu cha 31)

Kamisheni inaweza kuomba kwa jina lake eneo la ardhi kwa ujenzi wa msiki na madrassa katika eneo lolote la Zanzibar na baada ya kumalizika ujenzi wa msiki na madrasa hiyo itasimamiwa kwa masharti yaliyoidhinishwa na Kamisheni.

Hakuna mtu, mtoaji wa mali kama Wakfu au mdhamini wa mali hiyo atakayejenga au kusababisha kujengwa msiki hadi pale ambapo, kabla ya kufanya hivyo awe kwanza amepata ridhaa kwa maandishi ya Kamisheni kwa niaba hiyo baada ya kuiridhisha Kamisheni kwamba msiki uliopendekezwa umeekekewa fedha au unataka kuekewa fedha za kutosheleza ili kukidhi huduma zake za matengenezo kuuweka katika hali nzuri.

REJEA

Abdul Sheriff (1995), *The Records of the "Wakf Commission" As a Source of Social and Religious History of Zanzibar.*

Abdul-Hakim A. Issa (2007), *Wakf Commission*, paper presented in the workshop on "Strengthening the Legal Profession in Zanzibar", 24th – 25th February 2007

Abdulla Talib Abdulla (2011) *An Outlook of the Zanzibar Waqf Commission*, A Paper Presented in the Southern Africa Waqf Cadre Training Course Durban, South Africa 17th – 20th Feb. 2011.

عبد الرحمن أحمد عثمان (2007)، الوقف واثره في التنمية المجتمعية بالمجتمعات المسلمة، الخرطوم.

Amy Mardhatillah et al (2006), *Cash Waqf and Opportunity for Islamic Microfinance Institutions* (Case Study in Indonesia), Malaysia.

Ashfaque Ali (2002), *Socio-Economic Role of Awqaf in the Advancement of Muslims*. Awqaf, 3, 21-30.

Ashraf bin Md. Hashim (2007), *The Collection of Waqf through Insurance Companies: A Critical Analysis of the Malaysian Experience*, Oxford.

Adi Setia (2009), *Waqf & Civil Society in Islam: Reflections on Some Historical Case Studies*, A paper Presented in the Workshop on: Developing Managerial Skills of Waqf Professional Cadres, Pretoria, S. Africa (4-6 December 2009).

Baskan, B. (2002). 'Waqf System as a Redistribution Mechanism in Ottoman Empire', Chicago.

Habib Ahmed (Islamic Development Bank Group & Islamic Research and Training Institute, 2004). *Role of Zakah and Awqaf in Poverty Alleviation*, 8, 1-157, Jeddah, Saudi Arabia.

Issa H. Ziddy (2007), *Experience and Challenges of the Administration of Waqf Institution in Zanzibar*, paper presented in the International Conference on Developing Waqf Institutions for Sustainable Community Development and Poverty Eradication in Cape Town, Aug 17-19, 2007.

Juma Himid (1984) *Ripoti juu ya Utafiti wa Nyumba za Kamisheni*. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar.

Islamic Relief (2004), *Water Waqf Report 2004*. Retrieved <http://www.islamic-relief.com>.

Management and Development of Awqaf Properties: *Proceedings of the Seminar held on 7-19 Dhul Qada, 1404* (Jeddah, Islamic Research and Training Institute, Islamic Development Bank, 1987).

Monzer Kahf (1999), *Towards the Revival of Awqaf: A Few Fiqhi Issues to Reconsider*. (It was presented at the Harvard Forum on Islamic Finance and Economics, October 1, 1999, Harvard University, USA.

Muhammad A. Mbarouk et al (1998), *Existing Philanthropic Organization-WAKF is it a viable force?* NGORC, Zanzibar.

Murad Cizacka (2000), *Cash Waqf and Venture Capital Finance in Ontology of Islamic Banking and Finance*. Institute of Islamic Banking and Finance.

Muhammad Abdurrahman Sadique (2006), *Financing Waqf Projects: a Study of Past and Modern Structures Employed and the Relevant Shari'ah Aspects*. Malaysia.

Muhammad M. Abdulfatah(2004), *Simplified Islamic Jurisprudence Based on the Quran and the Sunnah*, Dar al Manarah, Egypt.

Proceedings of the *Awqaf & Zakah Seminar*, Durban, 1-4 September 2000, (South African National Zakah Fund); Islamic Research and Training Institute, Islamic Development Bank).

Reza Djojosugito (2007), *Bridging Waqf And Microfinance: Legal Challenges In Developing Waqf For Poverty Alleviation*, Vienna.

Saad S. Yahya (2007), *Compassion and Development: Addressing Social Infrastructure and Poverty Issues in East African Cities Through Wakf Endowments*, A Paper presented to the International Waqf Conference, Cape Town.

Sayed Khalid Rashid (October, 2003), *Current Waqf Experiences and The Future of Waqf Institution. Awqaf*, 5, 5-25.

Syed Khalid Rashid (2002), *Awqaf Experiences in South Asia*. New Delhi, India: Institutue of Objective Studies.

Tarak Abdallah (2009), *Globalization of an Ongoing Charity Towards a Global Agenda for Waqf Sector*, A paper Presented in theWorkshop on: Developing Managerial Skills of Waqf Professional Cadres, Pretoria, S. Africa (4-6 December 2009).

Tarak Abdallah (2011), *Waqf and State: The Neccesity of constructive Partnership*, Rabat

Wahbat Zuheyli (1989), *Al Fiqh Al- Islami wa Adilatuh*, Darul Fikr Damascus.

Zainul Abedien Cajee (2011), *Establishing An Awqaaf Foundation: Lessons from Awqaaf South Africa*, A Paper Presented in the Southern Africa Waqf Cadre Training Course Durban, South Africa 17th – 20th Feb. 2011.

Zanzibar Government Gazette Vol. CXVI No. 6211, *The wakf and Trust Commission Act, No. 2 of 2007*, 22nd June 2007.

Zulkifli Hasan (2007) *The Effectiveness Of The Administration Of Waqf Land In Malaysia*